

MABIRIKA YAVUJAYO



Bwana, naamini; Bwana, naamini,
Yote yawezekana; Bwana, naamini.

² Hebu na tubaki tumesimama kwa muda kidogo na kuinamisha vichwa vyetu. Bwana Yesu, tunajaribu kwa njia yetu nyenyekevu, kukuonyesha, kwa kuuimba huu, ya kwamba tunaamini. Na tunaomba, Bwana, ya kwamba sasa, ya kwamba Wewe utaendelea kutumegea Mkate wa Uzima, ukitupa kile tunachohitaji, kutoka kwenye Neno Lako. Kwa kuwa tunaomba hayo katika Jina la Yesu. Amina.

³ Ketini. Nina hakika kabisa, kama tungeweza, kama ningetamka sasa neno linalotosheleza kwa yote la “amina,” ya kwamba baraka tukufu za Mungu naomba zikae juu ya wasikilizaji hawa.

⁴ Nimeketi asubuhi hii na kusikiliza kwa makini ibada, nikafurahia shuhuda, njia mbalimbali ambazo kila mmoja alizo nazo za kujieleza wenyewe. Na kuwasikia wageni, Ndugu huyu wa Kibaptisti hapa ambaye amekuja kuomba msamaha kwa kufikiria hilo kidogo ni kosa. Ha—hakika ninathamini utu huo, mtu ambaye anaweza kuwa na utu wa kutosha, ama—ama muungwana vya kutosha, pia, kama akiwazia amefanya kosa. Kwa kweli hakuniomba mimi msamaha, si mimi aliyekuwa akiniomba msamaha, ilikuwa ni Mungu. Kwa hiyo na—nathamini hilo, mnaona. Mungu na ambariki ndugu yetu, na ndugu yake mwinjilisti.

⁵ Jamani, huyo Mbaptisti, mwajua, mimi mwenyewe nilikuwa mfuasi wa kanisa la Kibaptisti. Nilikuwa mfuasi wa Kanisa la Kimishenari la Kibaptisti. Ninapokuja miongoni mwa watu, ninajua jinsi mnavyojisikia. Nilijisikia vivyo hivyo, nimejaa tu kitu fulani ambacho si—sikuja.

⁶ Ninakumbuka tukio langu la kwanza la kumwona mpentekoste, ilikuwa ni huko Dowagiac, Michigan... Samahani, nilikuwa huko Dowagiac kwenye safari ya kuvua samaki, nami nilikuwa nikishuka kutoka Dowagiac, kuingia Indiana. Na kwa hiyo nikaona majina, ya “Yesu” kote kwenye magari na kadhalika, nami nikasikiliza ibada zao siku hiyo. Na kesho yake wakaniomba niende jukwaani, kusema maneno machache, nami nikafanya hivyo. Nami... Waliniuliza nilikuwa mfuasi wa kanisa gani, nami nikawaambia nilikuwa Mbaptisti.

⁷ Basi usiku huo walikuwa na mzee mmoja mweusi aliyekuwa anaenda kuhubiri, na hapana budi alikuwa katika miaka yake ya kumalizia ya themanini, naye akaja jukwaani. Jamaa huyo mzee, karibu iliwabidi wamwongoze wakati akitoka. Alikuwa ninii, alivaa moja ya hayo makoti marefu ya huduma, ule ukosi wa

mahameli, na mzingo mdogo tu wa nywele nyeupe umezunguka sehemu moja yake. Ndipo nikawazia, “Watu hawa wote hapa na wanatheolojia, watu mashuhuri, wangeruhusuje ibada hii ipewe jamaa kama huyo? Vema, mzee huyo alipaswa kuwa amekaa kwenye kiti mahali fulani, ameketi chini.”

⁸ Siku hiyo walikuwa wakihubiri juu ya yale Yesu aliyokuwa amefanya hapa duniani. Na, bali yeye alichukua, alichukua somo lake, ninaamini lilikuwa ni kutoka katika Ayubu...:7, 20, nisingekuwa na hakika kwamba Andiko ndilo hilo. Hata hivyo, hii ndiyo nukuu, ama sehemu yake, “Ulikuwa wapi nilipoweka misingi ya nchi, hapo nyota za asubuhi zilipoimba pamoja, na wana wa Mungu walipopiga kelele kwa furaha?” Naye akazungumza juu ya yale yaliyoendelea Mbinguni, wakati wao walipokuwa wakizungumza juu ya yale yaliyoendelea duniani.

⁹ Na mahali fulani, katika dakika tano hivi baada ya kuanza kuhubiri, yeye, Roho wa Bwana alimgusa, ndipo akaruka juu sana sakafuni na kugonganisha visigino vyake pamoja. Jamani, kulikuwa na nafasi kubwa sana, ilikuwa karibu nusu ya jukwaa hili; ndipo akatoka akaenda, kasema, “Hamna kabisa nafasi ya kutosha juu hapa ya mimi kuhubiria.”

¹⁰ Vema, nilikuwa na umri wa kama miaka ishirini wakati huo. Nikawazia, “Kama—kama hiyo itamfanyia hivyo mzee huyo, itanifanyaje mimi?” Kwa hiyo mnaona?

¹¹ Kwa ajili ya kuweka kila kitu katika utaratibu kwa ajili ya ndugu zetu wageni, kwamba kweli tunawakaribisha katika ushirika wetu. Ninaona, ninaamini walikuwa wamejulisha kuhusu kasisi mmoja anayeketi hapa, nafikiri; kwa kweli, nikiwa Mwairishi, watu wangu ni Wakatoliki. Na kwa hiyo kulikuwa na wengine kadhaa, Baptisti na wengineo. Huenda mlichanganyikiwa kidogo, muda mfupi uliopita. Niliona hakuna mmoja wa ndugu hawa aliyezungumza juu yake, bali nilifikiri ningejaribu kulinyoosha. Wakati Ndugu Shakarian... Baada ya mhubiri mzuri hapa kububujika sana kwa furaha, kwa kujua Kuja kwa Bwana kumekaribia sana, a—alinena kwa lugha isiyojulikana, kwetu. Na tuna watafsiri wanaotoa tafsiri. Ambapo, Maandiko yanasema, “Kama hakuna mtafsiri, basi na wanyamaze.” Lakini kama—kama wakinena kwa lugha kisha wazifasiri, inakuwa ni unabii. Kwa hiyo kuchanganyikiwa kudogo kwa—kwa hao wawili kwa wakati mmoja. Sasa, hilo halikuwa ni mchafuko hata kidogo, mnaona; kwa maana, mmoja wao alikuwa akitoa tafsiri, huyo mwingine alikuwa anatabiri. Unaona? Kwa hiyo hiyo ni... .

¹² Nilidhani ningewafanya ndugu zetu kuelewa, kama hawakuelewa, kwa maana mmoja wao alikuwa kwa usahihi akitoa ninii... Je! mliona kikomo cha wakati cha kila mmoja? Na huyo mwingine alikuwa amejazwa sana, yeye mwenyewe, hata Roho wa Mungu alikuwa akitabiri kupitia kwa mmoja;

akitafsiri, huyo mwingine alikuwa akitafsiri. Ili kwamba iweze kuwa dhahiri, ya kwamba ninyi... sisi hatuninii... Mara nyingine, kwa akili ya kawaida... Kama tu vile ndugu yetu wa thamani aliyeomba msamaha asubuhi ya leo. Inatatiza kidogo kwa mtu asiyefahamu. Bali kwa wale walio ndani, mashujaa wa vita tunavyopigana, mbona, tunafahamu jambo hilo, jinsi mambo haya yalivyo. Kwa hiyo nilifikiri tu ningesema jambo fulani kulihusu, kama ilikuwa ni sawa.

¹³ Sasa, ni—ninajua hapa si mahali pa kusema jambo hili. Lakini kwa kuwa kila mtu amekuwa akisimulia mambo madogo madogo, mimi... Mnajua, jamaa huyo alisema, yule mzee mweusi alisema, “hamna nafasi ya kutosha ya mimi kuhubiria.” Ninyi hamna *wakati* wa kutosha kwangu kuhubiria. [Kusanyiko linashangilia—Mh.] Kwa namna fulani ninachosha kwa maneno mengi.

¹⁴ Mtu fulani alisema siku moja, kasema, “Mhudumu mmoja alitokea, alikuwa mchungaji kanisani kwa muda wa miaka ishirini. Na daima alihubiri dakika thelathini kamili kila Jumapili asubuhi kanisani mwake.” Naye akasema, “Jumapili hii asubuhi, alihubiri kwa saa tatu.”

¹⁵ Na kwa hiyo halmashauri ya mashemasi ilimwita barazani, na kusema, “Mchungaji, tunakuthamini kweli.” Kasema, “Daima tunajua ya kwamba—ya kwamba unaitetea Biblia na haki Zake.” Na kisha wakasema, “Nawe daima unatusahihisha ili kwamba tuweze kujisikia wasio na doa na safi mbele za Mungu. Na kweli tunakuthamini, na tunaamini wewe ni mtumishi wa Mungu. Na hakika tulifurahia ujumbe huo asubuhi ya leo. Lakini,” wakasema, “kuna jambo moja tu tunalotaka kukuuliza juu yake.” Kasema, “Tulikupimia wakati, kama halmashauri ya mashemasi.” Wakasema, “Kila Jumapili asubuhi wewe huchukua dakika thalathini kamili, na leo ulichukua saa tatu.” Wakasema, “Sasa, kumbuka, tunathamini kila sehemu yake. Ulikuwa ni sawa.” Wakimfanya mzee huyo kujisikia vizuri, unajua.

¹⁶ Akasema, “Vema, ndugu, nitawaambia jinsi ilivyo.” Kasema, “Kila asubuhi ninapenda kwenye... ninapoitwa mimbarani,” kasema, “mimi huweka moja ya hizo Okoa Maisha mdomoni mwangu,” akasema, “na ninaimumunya tu.” Kisha kasema, “Okoa Maisha inapokwisha,” kasema, “inachukua tu dakika thelathini,” na kasema, “ndipo ninaacha kuhubiri,” Akasema, “Mwajua, asubuhi ya leo, nilifikiri nilipitiliza wakati kidogo. Niliitema, nilikuwa na kifungo mdomoni mwangu.” [Kusanyiko linacheke—Mh.]

¹⁷ Mimi sitaweka chochote ndani, kwa hiyo tunatumaini hatutapata vifungo mifukoni mwetu. Lakini sisi tunaninii... Ninatumaini hilo halikusikika ni la kukufuru hapa. Lakini ninaninii tu... Mwajua, hata Mungu ana ucheshi, mwajua.

¹⁸ Kwa hiyo tunashukuru sana kuwa hapa na kuwa na wakati huu wa ushirika, na—na tukiwa na majaliwa haya makuu ya kuvunja Mkate wa Uzima mara nyingine tena, katika njia yangu ndogo rahisi. Ninajua, kama wanatheolojia, kama vile yule mtu alivyozungumza hapa jana usiku kutoka Uingereza; jamani, ninachukia kuhubiri baada ya mtu kama huyo, nikiwa na elimu yangu ya darasa la saba. Lakini ninatumaini ya kwamba Mungu atawatafsiria maana iliyo moyoni mwangu. Unaona? Kama maneno yangu si sahihi; malengo yangu, ni—ninatumaini, ni sahihi.

¹⁹ Sasa hebu na tusome katika Maandiko. Wengi wenu mnapenda kufuatilia. Nami nitasoma asubuhi ya leo, kwa muda mfupi tu, kutoka katika Kitabu cha Yeremia, nabii, mlango wa 2, nami nitaanza sasa na kifungu cha 1.

Neno la BWANA likanijia, kusema,

Enenda ukalie masikioni mwa Yerusalemu, ukisema, BWANA asema hivi, Nakukumbuka, hisani ya ujana wako, na upendo wa wakati wa uposo wako; jinsi ulivyonifuata huko jangwani, na katika nchi isiyopandwa mbegu.

Israeli walikuwa utakatifu kwa BWANA; malimbuko ya uzao wake; wote watakaomla watakuwa...na hatia; uovu utawajilia; asema BWANA.

Lisikieni neno la BWANA, ninyi nyumba ya Yakobo, na ninyi, jamaa zote za nyumba ya Israeli.

BWANA asema hivi, Baba zenu waliona dhuluma gani kwangu, hata wakafarakana nami, wakafuata ubatili, nao wakawa ubatili?

Wala hawakusema, Yuko wapi BWANA, aliyetutoa katika nchi ya Misri, na akatuongoza jangwani, katika nchi ya ukame na mashimo, katika nchi ya kiu na ya vivuli vya mauti, katika nchi ambayo ndani yake hapiti mtu, wala...haikaliwi na watu?

Nami nikawatia katika nchi ya shibe, mpate kula matunda yake na mema yake, lakini ninyi mlipoingia katika nchi ile, mliitia unajisi nchi yangu, na urithi wangu mliufanya kuwa chukizo.

Makuhani hawakusema, Yuko wapi BWANA? Wala wana-sheria hawakunijua; na wachungaji nao waliniasi, nao manabii walitoa unabii kwa Baali, wakafuata mambo yasiyofaidia kitu.

Basi kwa ajili ya hayo nitaninii...nitateta nanyi, asema BWANA, nami nitateta na watoto wa watoto wenu.

Maana,...mpaka nchi hii ya Kitimu, mkaone; tumeni watu waende kule Kedari, mkafikiri sana; mkaone kwamba jambo kama hili limekuwa wakati wo wote.

Je! Taifa wamebadili miungu yao, ingawa...siyo miungu? Lakini watu wangu wameubadili utukufu wao kwa ajili ya kitu kisichofaidia.

Enyi mbingu, staajabuni kwa ajili ya jambo hili, muogope sana, . . .kuwa ukiwa sana, asema BWANA.

Kwa maana watu wangu hawa wametenda maovu mawili; wameniacha mimi, niliye chemchemi ya maji ya uzima, na wamejichimbia mabirika, mabirika yavujayo, yasiyoweza kuweka maji.

²⁰ Bwana na aongeze baraka Zake kwa kusomwa kwa Maneno Yake. Nami ningependa ku—kuchukua somo la hayo, kama, *Mabirika Yavujayo*.

²¹ Wakati, tukisoma Andiko hili asubuhi ya leo; ambapo, Maandiko yote yana pumzi. Nasi tunakuja kwenye Nyumba ya Bwana kwa ajili ya masahihisho na kufahamu. Na mara nyingine tunapoona ninii . . . jambo lolote dogo lililoko njiani.

²² Kama vile mtu huyu mwanajeshi, muda mfupi uliopita, alivyokuwa akituzungumzia na kusema ya kwamba mambo fulani, ya kwamba labda huenda ikawa katika nchi nyingine ina kombora fulani, ama—ama wazo kama hilo, nasi hatuna budi kupata kitu cha kukabiliana na hicho katika—katika mkakati wa kijeshi.

²³ Vema, jambo lilo hilo linatenda kazi kanisani, kwenye parokia ambako mtu anahubiri, ama kama yeye ni mwinjilisti hudumani. Anapoona maasi, na jambo fulani ambalo ndio tu linaanza, likiendelea, linapoibuka ama chochote kile; ni mtu huyo, kama yeye ni mtumishi wa Mungu, kuzuia jambo hilo mbali na mioyo ya watu hivi kwamba watajiepisha nalo. Nasi hatutaki jambo hilo litukie, kwa sisi kuingia kwenye mahali kama hapo.

²⁴ Sasa, katika wakati wa Yeremia hapa, unabii wake, ilikuwa ni kama miaka sitini tangu kifo cha—cha Isaya—Isaya. Nao walikuwa wamekaa karibu miaka sitini bila nabii mkuu. Kulikuwako na Habakuki na baadhi ya wale manabii wadogo wadogo, bali Isaya alikuwa ndiye nabii mkuu wa mwisho. Nao hao watu walikuwa, mnamo wakati huu, hawakuwa na mtu yeyote wa kuwaita watoke. Walikuwa wameenda pepe. Hata hivyo, walikuwa ni watu wa Mungu, walikuwa wameenda pepe wakaingia katika hali hii sasa ambayo—ambayo tunawakuta nayo, wakati Yeremia alipokuja kuwatabiria. Naye Yeremia pia alikuwa . . . Alitabiri kabla ya ule uhamisho, na pia alienda uhamishoni pamoja nao.

²⁵ Na halafu, bila shaka, Danieli alikuja baada ya Yeremia. Naye Danieli alisema ya kwamba alikuwa na ufahamu, kwa Maandiko, wa ile miaka sabini ambayo walipaswa kuwa kule.

26 Kwa kweli, kulikuwa na nabii mwingine miongoni mwao, ambaye alitaka kutengeneza nira hii, naye akaiweka shingoni mwake, ya kwamba lingekuwa ni jambo dogo, kwamba, “Katika miaka miwili, vema, Mungu atawarudisha wote,” bali Yeria alijua tofauti na hilo. Nasi tunajua ni jambo gani lililompata nabii aliyetabiri uongo, yeye alikufa mwaka uo huo. Kwa hiyo Mungu asingemruhusu kusimama.

27 Na sasa pia tunaona hali za watu katika siku ile. Sasa siwataki mnielewe vibaya (mi—mimi sikusudii) katika yale ninayokusudia kusema hapa, baadhi ya Maandiko na mihtasari midogo.

28 Ilikuwa kwamba haikunibidi ku—kuandika Maandiko yangu na kadhalika. Bali baada ya mimi kupita umri wa miaka ishirini na mitano mara ya pili, vema, si—sikumbuki kama nilivyokuwa nikikumbuka, kwa hiyo mimi huandika Maandiko na kwa namna fulani ninajua, kutokana na hayo, mahali ninakoelekea. Halafu basi muda mwingi sana nikiwaombea wagonjwa, na kadhalika, kisha ninatoka na kusafiri, kweli sina wakati hasa wa kusoma kama inipasavyo.

29 Sasa, lakini nabii huyu mkuu wa siku hii, alikuwa ni Yeria, naye alikuwa kitu mithili ya Amosi na wengi wa manabii hao wengine walioinuka. Alighadhabika wakati alipoona hali za taifa. Sasa kulikuwa na sehemu. . .

30 Mara nyingine unapozungumza juu ya taifa, huenda ikawaziwa kwamba inaelekezwa kwenye kundi fu—fulani. Sivo. Ni picha ya kijumla ya taifa. Nasi tunaona, leo, hali inayofanana sa—sana leo na ilivyokuwa katika siku za Yeria, ya kwamba taifa lenyewe, kwa jumla, limeingia, karibu, katika ibada ya sanamu; kwa namna fulani, ningesema, limemwacha Mungu. Na kwa kufanya jambo hilo, imekuwa ni udhaifu wa mimbarani. Kwa sababu, kama mimbara ingalidumu kuwa sawa, na pamoja na Neno la Mungu, Mungu angekuwa kwenye kila kanisa kama vile anavyotenda kazi miongoni mwetu hapa. Bali wameondoka kwenye jambo hilo. Na hilo ndilo jambo ambalo ni—ninataka kuzungumzia asubuhi ya leo. Na sasa tunaona ya kwamba hiyo ni kweli kabisa katika kila kipindi cha wakati.

31 Ninaamini ilikuwa ni Amosi, kama nilivyoelezea habari zake muda mfupi uliopita, ya kwamba alisema yeye hakuwa “nabii, wala mwana wa nabii.” Lakini alisema, ya kwamba, “Simba akinguruma, ni nani asiyeweza kuogopa?”

32 Na kama mtu yeyote alipata kumsikia simba halisi akinguruma huko nyikani, hawa mnaowasikia katika vitundu hapa wanalia tu kama paka. Bali mmoja akilia huko nyikani, kila kitu husikiliza. Nimelala huko msituni, kuwawinda. Naye ndiye mfalme wa wanyama, na, huyo simba anaponguruma, hata mende hunyamaza, kila kitu hunyamaza. M—mbwa mwitu

na—na fisi wakilia, na wanyama wengine, na vilio vya nyani na tumbili, mende, ni vigumu kujisikia ukiwaza; bali huko mbali hebu simba na angurume, na kila mende ataacha kupiga makelele. Unaona, kila kitu kinamwogopa. Hata hivyo, kuna vitu vingi vinavyoweza kumwua, bali anatambuliwa kama mfalme miongoni mwa wanyama.

³³ Yeye alisema, “Simba anaponguruma, ni nani asiyeweza kuogopa?” Alisema, “Basi Mungu amenena, ni nani asiyeweza kutabiri?”

³⁴ Na hiyo, nafikiri, hali hiyo inakabiliana na changamoto tena leo. Mungu amenena. Unaona? Nasi tunaona maandiko ya mkono kwenye ukuta, kwa hiyo ni rahisi sana kutabiri na kuona ya kwamba tuko katika wakati wa mwisho.

³⁵ Nasi tunamwona Mungu, kutoka kila sehemu ya madhehebu, kote kote kutoka kwenye Ukatoliki, kupitia kwenye makanisa yote ya kiprotestanti, Wabudha na chochote kile, kutoka India, na chochote kile. Yeye anawaita watu Wake waje pamoja, anawakusanya pamoja. Nami ni—nina furaha sana kwa ajili ya jambo hilo, kuona siku hii ikija. Sasa sisi. . . ni—ni siku kuu, moja ya majaliwa makubwa sana.

³⁶ Hilo, kama ingelinibidi kuninii, kama ningelijua kabla hakujakuwako na ulimwengu, wakati tulipokuwa nafsi sehemu ya Mungu, jinsi tulivyo, kwa kuwa tulikuwa pamoja Naye kabla ya kuwekwa misingi ya dunia. Kwa sababu, kuna aina moja tu ya Uzima wa Milele, na huo ni Mungu. Nasi ni sehemu Yake. Hatukuwa zaidi sana ya kwamba tungejua na—na tungeweza kuwazia, na tungekuwa kiumbe chenye uhai; bali tulikuwa katika mawazo Yake ya vile tulivyokuwa, kabla ya kuwekwa misingi ya dunia. Kwa sababu, sisi ni sehemu Yake, kama vile mwanangu alivyo sehemu yangu, nami ni sehemu ya baba yangu, na kadhalika. Sisi ni wana na binti za Mungu, kwa kujua Kwake kabla.

³⁷ Na kule nyuma, kama ningeweza kufahamu kama ninavyofahamu sasa, na ningeweza kuangalia kwenye kitambo chote cha wakati, Naye angaliniambia, “Unataka kuishi wakati gani?” Ningalisema wakati huu sasa hivi, kwenye magharibi tu ya mwi—mwisho wa historia ya ulimwengu, na kule kuja kwa Ufalme wa Mungu kuanzishwa duniani. Nafikiri ndio wakati wenye utukufu sana wa nyakati zote, ni sasa hivi.

³⁸ Tunaona hapa ya kwamba Israeli wanashtakiwa na nabii, wakati Mungu alipokuwa amemtia mafuta na kumtuma, walishtakiwa dhambi mbili kuu. Nasi tunataka kuzungumzia juu ya mambo hayo mawili waliyokuwa wamefanya. Na, kutokana na hayo, tunataka kufaidika nayo. Sasa, walikuwa wamemwacha Mungu, Chemchemi ya maji ya uzima, na walikuwa wamejichimbua mabirika. Walikuwa wameacha kitu ambacho Mungu alikuwa amewapa, na wakawa wamejichimbua

kitu walichokuwa wamekifanya wenyewe. Na mabirika haya, unaona, yeye alikuwa, yalikuwa yamepasuka na yalikuwa yakivuja.

³⁹ Sasa, birika lililopasuka haliwezi kuweka maji. Litavuja. Nililelewa shambani, nami ninajua jinsi birika la siku nyingi lilivyo, na shida tunazopata kwake.

⁴⁰ Na birika hili linalovuja ni picha nzu—nzuri sana, nafikiri, ya siku hii, ya kwamba wakati kila kitu (chetu) ambacho tumejaribu kufanya, kuwaunganisha watu, kuwakusanya watu, kuyaunganisha makanisa, limekuwa daima kwenye anga za majaribio ya kiakili. Tumejaribu kuwafanya Wamethodisti wote kuwa Wabaptisti, na vinginevyo, na madhehebu mbalimbali. Wala huo haukuwa ni mpango wa Mungu, kwanza.

⁴¹ Mungu ana mahali pamoja tu pa kukutania. Alisema kule kwenye Kitabu cha Kutoka, ya kwamba, “Nimepachagua mahali pa kuweka Jina Langu, na hapo ndipo mahali pekee nitakapokutana na watu.” Naye alikuwa amechagua mahali pa kuweka Jina Lake. Na mahali alipoliweka Jina Lake, hapo ndipo alipokutana na Waisraeli. Yeye ana mahali anapokutana na kanisa Lake leo, Naye alilichagua Jina hilo, na jina hilo ni Yesu Kristo. Na hapo ndipo anapokutana na mwaminio wa kweli, wakati akiwa katika Yesu Kristo. Hapo ndipo Mungu alipochagua kuweka Jina Lake.

Unasema, “Ati Jina la Mungu?”

⁴² Yeye alisema, “Nilikuja katika Jina la Baba Yangu.” Kwa hiyo hapo ndipo Mungu alipoweka Jina Lake, ilikuwa ni katika Kristo. Na katika Kristo ndipo sote tunapoweza kukutana chini ya Damu iliyomwagika, na hapo tunapata ushirika halisi, wa kweli.

⁴³ Mungu aliweka mpango Wake hapo mwanzo, katika bustani ya Edeni, mahali ambapo ndipo angekutana na mwanadamu, na hapo hapakuwa ni juu ya ufahamu wa kiakili; kama ilikuwa hivyo, basi Hawa alikuwa kwenye mpango Wake sawasawa kabisa. Lakini tunajua ya kwamba kukubali kwake wazo la kiakili la Shetani, “Hakika, Mungu hatafanya hivyo,” bali Mungu alisema angefanya hivyo! Na kwa hiyo basi Yeye alichagua mahali pa ukombozi, na palikuwa ni kwa Damu, wala si kwa wazo la kiakili.

⁴⁴ Kwa hiyo tunapoteza tu wakati, lakini ndiyo tabia tu ya mwanadamu ya kwamba—ya kwamba watu watajaribu ku—kufanya jambo hilo. Kama tungelikuwa na wakati, tungeliweza kulivunja katika vipande vingi, bali sitaki kifungo hicho. Kwa hiyo tutajaribu tu kulifanya rahisi iwezekanavyo, “mabirika yavujayo.” Nasi tunaona ya kwamba yakini i—imetendeka tena, ni picha halisi ya wakati wetu tunaoishi, katika kujaribu kwetu kote.

⁴⁵ Wala sipuuzi kila jitihada ambayo mtumishi yeyote wa Mungu, ambaye hata hutaja Jina la Yesu Kristo. Anapaswa kuheshimiwa hata kwa ajili ya kulitaja tu Jina Lake kwa uchaji na heshima. Na mifumo mikuu ya kiinjilisti ambayo imepita duniani, na kadhalika, katika siku hizi za mwisho, nafikiri, bado kamwe hatutaweza kuwafanya watu wawe katika moyo mmoja mpaka tutakapowaweka chini ya Damu ya Yesu Kristo. Hapo ndipo mahali pekee tutakapoweza kuwa salama.

⁴⁶ Mtu fulani alinipigia simu si muda mrefu uliopita, kutoka huko Mashariki, naye akasema, “Ndugu Branham, ninasikia ya kwamba umehamia hu—huku Arizona, na ukafanya huko ma—mahali palipo na usalama.” Na kama mnavyojua jinsi ujumbe ulivyokuja, na Bwana akaniambia kile kingetukia huko Alaska, na jinsi ambavyo hali ingekuwa huko chini kupitia California, na imekuwa tu namna hiyo. Wao walisema, “Sasa kama hiyo inatikisika, na kila kitu, iko wapi zoni ya salama?”

⁴⁷ Nikasema, “Kuna zoni moja ya salama niijuayo. Hiyo ni katika Kristo. Kwa kuwa wale walio katika Kristo, wataninii . . .” Ndio pekee niwajuao.

⁴⁸ Sasa Yereimia aliitwa, pia, “nabii aliaye.” Na kwa sababu, ninaamini, kile kilichomfanya nabii huyu alie—alie, hasa, ilikuwa ni kwa sababu yeye akiwa ni nabii (na Neno la Bwana linawajia hao) na kuwaona watu wakitembea katika mapokeo yao wenyewe, na walifikiri walikuwa wako sahihi, wala hapakuwapo na njia hata kidogo ya kuwageuza.

⁴⁹ Kwa kuwa, walikuwa wakienda moja kwa moja uhamishoni, kwa maana tunajua unavuna unachopanda, haidhuru wewe ni nani, kile ulicho. Nasi kama taifa tumevuna . . . ama tumepanda, hasa, na hatuna budi kuvuna. Nitakapokuwa ninazungumza kesho, Bwana akipenda, alasiri, juu ya *Utungu wa Kuzaa*; nami—nami ninagusia hilo kwenye huo, ya kwamba hatuwezi kuepuka kwa vyovyote. Hatuna budi kuvuna tunachopanda.

⁵⁰ Na kama Mungu angetuachilia tuendelee na upotovu wetu wa Ukristo leo, na kuwapotosha watu katika mambo haya yanayoitwa Ukristo, kama vile Ndugu Moore alivyosema wakati mmoja, “Yeye angewajibika kimaadili kuifufua Sodom na Gomora, na kuomba msamaha kwa kuwateketeza kwa moto.” Hiyo ni kweli, kwa maana Mungu angali ni mwenye haki. Na mahali ambapo hapana haki; utakatifu Wake na Neno Lake hu—huhitaji ya kwamba awafanye watu wavune waliyopanda, nasi itatubidi kufanya hivyo.

⁵¹ Sasa angalia kwamba walikuwa wamemwacha Yeye, Chemchemi ya maji ya uzima, nao walikuwa wamejichimbua mabirika.

⁵² Sasa huenda ikawa kuna mtu hapa ambaye hangejua birika ni kitu gani. Birika ni tangi lililotengenezwa na mwanadamu linalojaribu kupachukua mahali pa kisima. Ni kitu ambacho

mtu fulani alichimba. Na ni wangapi wanaojua birika ni kitu gani? Sawa. Vema, watu wengi wa mashambani hapa asubuhi ya leo. Kwa hiyo wao...Ninakumbuka birika lile la kale mahali pale, jinsi lilivyoonekana, nami daima niliogopa kunywa kutoka kwenye kitu hicho. Lilikuwa ni tangi lililotengenezwa na mwa—mwanadamu. Wala haliwezi kamwe kutegemewa. Huwezi kutegemea birika.

⁵³ Sasa kitu chochote ambacho mwanadamu hufanya kwa kawaida si kizuri sana. Lakini kama tu vile Bwa—Bwana alivyoweka wakati katika—katika—katika duara lake, na dunia kuzunguka; kila mwaka, kila wakati inapopita, kila siku, kila saa, na na jua likitua, wala halikosei. Lakini saa nzuri sana tunazoweza kupata, zitakosea dakika nyingi katika muda wa mwezi mmoja, hapana shaka. Lakini, unaona, kila kitu anachofanya Mungu ni kikamilifu, na kile mwanadamu anachofanya si kikamilifu. Kwa hiyo kwa nini ukubali kile mwanadamu anachofanya, wakati unaweza kupata kilicho kikamilifu?

⁵⁴ Daima nimesema hivyo kuhusu sisi Wapentekoste. Unaona, tunajua, wala sisi si—sisi bila shaka hatuko nje ya utaratibu wa mwenendo, wa Mungu, hatuamini; bali pia tunajua ya kwamba miongoni mwetu tuna watu wanaojaribu kumwiga mtu mwingine. Hiyo ni tabia ya ubinadamu tu. Watu watajaribu kufanya jambo hilo. Walifanya hivyo katika Biblia, “Mmoja, ‘Mimi ni wa Paulo,’ ‘Mimi ni wa Sila,’” na kadhalika. Lakini, wao, walijaribu kuiga yale mtu mwingine aliyofanya ama anayofanya.

⁵⁵ Lakini kwa nini ukubali uigaji wa uongo, wakati mbingu zimejaa jambo la kweli, wakati “ahadi hii ni kwa ajili yenu na kwa watoto wenu”? Kwa nini tukubali kitu ambacho kilikuwa ni cha tofauti? Kwa nini tuchukue kanuni fulani ya imani ama fundisho fulani la sharti, wakati Biblia ni Neno la Mungu lisiloghoshiwa? Kwa nini tujaribu kuongezea ama kuondoa, wakati Bwana Yesu alisema katika Ufunuo 22:18, “Mtu yeyote atakayeondoa Neno moja Kwake, ama kuongezea neno moja Kwake, sehemu yake itaondolewa katika Kitabu cha Uzima”?

⁵⁶ Wakati Mungu alipoiweka jamii ya binadamu duniani kwa mara ya kwanza, Yeye aliwaambia waishi kwa Neno Lake. Sasa Neno la Mungu ni kama mnyororo, unavuka jehanamu Nao; na mnyororo wake uko tu katika kipeo cha ubora wake kwenye kiungo chake kilicho dhaifu sana, naye Mungu anatutaka sisi tudumishe kila Neno Lake. Sasa hiyo ilikuwa ni mwanzoni mwa Biblia; kuvunja tu Neno moja, kuliitumbukiza jamii ya binadamu katika giza la mauti.

⁵⁷ Yesu alikuja katikati ya Biblia, na akasema kwamba, “Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno.” Si sehemu tu ya

Maneno, ama tisini na tisa kwa mia; bali kwa kila Neno, kama tu vile Hawa na Adamu walivyokuwa.

⁵⁸ Na mwishoni mwa Biblia, Ufunuo 22:18, akasema kwamba, “Mtu yeyote atakayeondoa Neno moja kutoka Kwake, ama kuongeza Neno moja Kwake!”

⁵⁹ Basi kwa nini tunahitaji kuingiza Hapa wazo la mambo ya mtu fulani, wakati hili ndilo Wazo la Mungu Mwenyewe kulihusu? Tunataka kuchukua yale aliyosema. Na pia imeandikwa, “Neno la kila mtu na liwe ni uongo, na Langu liwe ni Kweli.”

⁶⁰ Hiyo ndiyo shida ya nabii huyu. Katika siku za Yeremia, yeye alikuwa ni nabii, yeye alikuwa na Neno la Bwana. Na jamaa huyu alikuwa akijaribu kuingiza kitu fulani ndani Yake, sasa haliwezi kutegemewa. Nami ninayafananisha matangi haya sasa na mifumo hii ambayo tumejaribu kuchukua, na kupachukua mahali pa Neno la asili la Mungu.

⁶¹ Kwa kuwa, hakuna kitu kinachoweza kupachukua mahali pake. Ni Mungu. “Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa miongoni mwetu.” Na Waebrania 13:8, ilisema, “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.” Tunawezaje kuepa jambo Hilo? Halina budi kuwa ni Kweli. Yeye angali ni yeye yule. Ni yeye yule katika kila kanuni.

⁶² Hiyo ndiyo sababu mnaufurahia Huo, ninyi Wabaptisti na Wamethodisti, na Wakatoliki na Wapresbiteri, na kadhalika, mnaufurahia ule Uwepo. Mahali fulani, ndani yenu, mmemkubali Mungu. Labda pengine katika njia ya kiakili, pengine mmezihisi Nguvu za Mungu, nawe ni mtumishi wa Mungu; lakini wakati unapoweza kuingia katika Mungu kweli, na kutambua mahali pako ndani Yake, kama mwana au binti wa Mungu, hilo ndilo linalosababisha changamko hilo kuu kwako, ambalo Mungu alikukusudia kuwa nalo.

⁶³ Sasa tunaona katika Marko Mtakatifu, mlango wa 16, Yesu hakusema, “Enendeni ulimwenguni mwote, m—m—mkafundishe.” Yeye alisema, “Enendeni mkaihubiri Injili.” Kuhubiri Injili, ni, kuonyesha Nguvu za Roho Mtakatifu! “Enendeni ulimwenguni mwote, mkaonyeshe Nguvu za Roho Mtakatifu.”

⁶⁴ Nilikuwa nikizungumza na ndugu fulani, mmoja wa wadhamini kwenye...mkutano wangu huko India, huko Bombay kule, Afrika Kusini na mahali mbalimbali, ambako wamishenari walikuwa wamelifundisha kama neno ama kama wazo la kiakili. Bali siku moja mkutanoni, wakati Roho Mtakatifu aliposhuka, Yeye Mwenyewe, na kuwaokoa wananchi elfu thelathini wanaovaa mablanketi kwenye wito mmoja wa madhabahuni, na moja kwa moja mahali pale pale walipokuwa wamesimama. Wanawake wakisimama pale, waliokuwa uchi

karibu kama walivyokuwa walipokuja ulimwenguni, na dakika ile ile walipoinua mikono yao kumpokea Kristo . . .

⁶⁵ Ndipo Roho Mtakatifu alishuka mahali hapo na kuwaponya watu elfu ishirini na watano wakati mmoja, wakatoka kwenye viti vya magurudumu, vitanda vidogo na machela. Meya wa mji huo akaniambia, kesho yake, niangalie malori haya yaliyojaa yakishuka kwenda mtaani.

⁶⁶ Hao wanawake wakisimama pale, uchi, bila kujua walikuwa uchi. Lakini mara Roho Mtakatifu alipowagusa, walikunja mikono yao waondoke mbele ya wanaume wao.

⁶⁷ Nami ninashangaa jinsi ambavyo sisi hapa Marekani tunavyojiita taifa la Kikristo, na katika Uwepo wa Mungu; na kila mwaka sisi, wanawake wetu, wanazidi kuzivua. Nanyi mnapaswa kuwa mkivaa nyingi zaidi. Na kadiri mnavyomvaa Kristo, ndivyo mtakavyozidi kujua hali zenu. Mara nyingine ninaona jinsi watu wanavyofanya mtaani, ninashangaa kama kweli wao wana akili timamu. Inaonekana kana kwamba hawatambui ya kwamba wanapofanya mambo hayo, yale wanayofanya, wanajifanya kuwa chambo cha ibilisi, na kuwapeleka watu kuzimu. Hiyo ni kweli. Lakini ulimwengu uko katika upotovu kama ulivyokuwa katika siku za Yeremia.

⁶⁸ Sasa turudi kwenye lile birika. Sasa, birika hili haliwezi kutegemewa kwa sababu haliwezi kujijaza. Nalo inabidi litegemee mvua za mahali hapo kulijaza, mvua za mahali hapo ama uamsho wa mahali hapo, kupata uamsho mdogo *hapa* na uamsho mdogo *pale*, ama chochote kile, lipate kujaa. Kwa hiyo haliwezi kutegemewa. Haliwezi kujijaza. Halijitoshlezi, lenyewe. Haliwezi. Nalo halina budi kutegemea mvua; ipate kulijaza.

⁶⁹ Basi hebu na tuone wapi li—linapata mvua yake, mahali linapopata maji yake, birika hilo. Yanatoka juu ya maghala, vibanda, ambako uchafu wote na mavumbi vinavyopeperushiwa kule juu, vinachukuliwa moja kwa moja na mvua, na moja kwa moja vinaingia kwenye birika hilo, tangi la kujitengenezea. Linakuwa karibu kama shimo la maji machafu. Na yanazoa kutoka juu ya mapaa ya ghala ambapo wanyama wote, harufu ya maeneo ya ardhi ya maghala, na kadhalika, na kulundikana chini. Na hewa inapulizia kuleta ma—mavumbi na takataka zilizoko juu ya ghala, ndipo mvua ya mahali hapo inakuja na kuyazoa, hiyo mvua, moja kwa moja.

⁷⁰ Na ndipo maji hayo yanabebwa na kihori cha kujitengenezea kupitia kwenye mlizamu wa kujitengenezea, yakaingia kwenye tangi la kujitengenezea. Na ndipo yanapofika mle, ni machafu, ni machafu sana hivi kwamba inakubidi kuweka kitambaa cha kuchujia juu yake, la sivyo usingeweza kuyanywa. Sasa, unaona, yanachukuliwa kutoka kwenye paa, na kihori cha kujitengenezea, mlizamu wa kujitengenezea, yakaingizwa

kwenye tangi la kujitengenezea. Halafu lina chujio la kujitengenezea juu yake, kuona kwamba baadhi ya wadudu na kadhalika wanachujwa.

⁷¹ Sasa, sasa tunaona, katika siku hizi chache baada ya maji kukaa pale, katika madhehe- . . . haya ya kujibunia, ama tangi. Samahani. Samahani. Vema. Baada ya—baada ya kuzolewa, kwa kila namna ya theolojia na kadhalika kuingizwa ndani yake; sasa tunakuja kuona, yakiisha kukaa pale siku chache, yanatuama.

⁷² Na mtu yeyote anajua, katika historia ya kanisa, wakati Mungu anapotuma kitu fulani, ujumbe, nao unatoka usioghoshiwa moja kwa moja toka kwa Mungu, basi baada ya u—uhai wa huyo mwanzilishi (ama chochote kile, mnamwita mtengenezaji, ama chochote mnachotaka kusema juu yake), baada ya kifo chake, ndipo wanabuni mfumo fulani na wanaunda madhehebu. Na mara wanapounda dhehebu kutokana na huo, linakufa papo hapo. Haliinuki tena. Lilifanya hivyo kila wakati, huko nyuma, huko nyuma kabisa.

⁷³ Katika kumheshimu kasisi huyu wa Kikatoliki anayeketi hapa; wakati Mungu alipoliundia kanisa dhehebu . . . ama, si kuliundia dhehebu, Mungu kamwe hakuliundia kanisa dhehebu. Yeye hayuko kwenye shughuli za namna hiyo. Yuko katika kuzaliwa, si kuunda madhehebu, kwa hiyo Mungu alipolanzisha kanisa kwenye Siku ya Pentekoste. Na halafu hatimaye huko Nikea, Rumi, wao waliliundia madhehebu, na hapo ndipo lilipopoteza Nguvu zake.

⁷⁴ Halafu tunashuka kuja kwenye matengenezo ya Kilutheri, nayo yalikuwa ni jambo kuu. Neno la Mungu lilitolewa, “Wenye haki wataishi kwa imani.” Na walipofanya hivyo, badala ya kuinuka, wote kwa pamoja, wote pamoja wakisonga mbele, waliunda kanisa la Kilutheri, wakijitenga na kundi hili, na ndipo likafa.

⁷⁵ Ndipo Mungu akamwinua John Wesley, akiwa na utakaso, ule ujumbe wa kazi ya pili ya neema, na lilikuwa ni jambo zuri sana. Lakini baada ya Wesley na Asbury, waliliundia dhehebu, nalo likafa.

⁷⁶ Ndipo wakaja Wapentekoste wakiwa na kurudishwa kwa karama. Walikuwa wakifanya vyema, ni jambo gani lililotukia? Waliliundia dhehebu nalo likafa. Kweli kabisa.

⁷⁷ Sasa katikati ya haya yote, Mungu angali anaita mabaki kutoka katika kila moja ya vizazi hivyo. Hakika anaita. Na ni wakati wetu wa kutoka, wa kukusanyika pamoja. Na hivyo ndivyo ninavyofikiri, Wafanyabiashara wa Full Gospel wamechukua sehemu kubwa katika kuvunja kuta hizi, na wakisema ya kwamba, “Hakuna tofauti kati yetu. Hebu na tukutane na kumwabudu Mungu chini ya kanuni moja, sio chini ya dhehebu fulani.” Kama lingekuwa ni dhehebu, ningetoka kwenye jukwaa hili sasa hivi. Sina uhusiano wowote nalo.

78 Jambo ni kwamba, inapaswa iwe ni ushirika, wala si ushirika wa kanuni fulani za imani. Bali ni ushirika ndani ya Kristo, kwa nguvu za kufufuka Kwake, hicho ndicho kitu kinacholeta Uzima. Kinaleta kuzaliwa.

79 Na kabla kuzaliwa kuweza kuja, tunatambua hakuna budi kuwe na mauti kabla ya kuzaliwa. Na uzazi ni mchafuko, sijali ni kuzaliwa kwa namna gani. Kama ni katika kizimba cha nguruwe, ama—ama popote pale, ni mchafuko. Na ndivyo kulivyo Kuzaliwa upya, kunakufanya utende mambo ambayo kwa kawaida usingewazia ungeyafanya. Lakini unapokuwa tayari kuifia nafsi yako, ndipo unazaliwa mara ya pili, kiumbe kipya katika Kristo Yesu, ndipo mambo, yanafunguka na maisha yanakuwa sura mpya kwako, kwa kuwa umekubali Utu wa Yesu Kristo, wala si nadharia fulani wala kanuni fulani za imani.

80 Ama, hata kwa Neno lililoandikwa, halina budi kuhuishwa na Roho Mtakatifu. Haidhuru una theolojia kiasi gani, ipo hapo imekufa. Ningeweza kuwa na konzi ya ngano; mpaka itakapofikia kwenye kiwango ambacho inaweza kuhuishwa, ngano hiyo haitaishi kamwe. Nawe unaweza kuwa na digrii ya udaktari, Ph., LL., chochote unachotaka; bali mpaka Roho Mtakatifu atakapokuja juu ya hilo na kulihuishwa kwako, kama tukio la binafsi pamoja na Mungu, basi hiyo ngano haifai kitu. Masomo yako ni bure.

81 Kama vile huyu Mwingereza alivyosema hivi majuzi usiku hapa, nilishangazwa sana na jambo hilo. Kisomo chote alichokuwa nacho, kama vile Paulo, ilimbidi kuyasahau yote aliyojua, kusudi ampate Kristo, kufanya mambo ambayo alifikiri asingeyafanya.

82 Lakini hivyo ndivyo Mungu anavyofanya, Yeye hutushusha katika mfumo wetu wa elimu. Si kwamba eti ninajaribu kuunga mkono ujinga, bali ninajaribu kuwaambia tofauti ya hayo. Elimu kamwe haiwezi kuleta Uzima. Inahitajika Roho wa Mungu kuleta Uzima, na Uzima huo haupaswi kutokana na uamsho tu wa kiakili. Unapaswa kutoka katika Biblia, uamsho wa Neno, na Neno hilo ni lile lile jana, leo, na hata milele. Na wakati linapoanguka leo, na linahuishwa, unapata matokeo yale yale uliyopata katika Matendo 2. Kweli kabisa. Siku zote limefanya hivyo, na daima litafanya hivyo, kwa sababu Roho wa Mungu ndiye anayetengeneza mazingira.

83 Inahitaji mazingira kufanya mambo. Hiyo ndiyo sababu ninyi wanaume mnafundishwa daima, “Waleteni watoto wenu hapa.” Vema, bila shaka hiyo ni kweli. Nilifurahi kumwona binti yangu, Rebekah, akiingia na kuketi, dakika chache tu zilizopita. Baadhi yenu mliniona nikimkonyezea mwanamke fulani jicho, ilikuwa ni binti yangu, kwa hiyo aliingia na kuketi chini. Ninamtaka apokee ubatizo wa Roho Mtakatifu, na hiyo

ndiyo sababu yeye yupo hapa mkutanoni. Hilo ndilo kusudi la jambo hili. Inahitaji mazingira.

⁸⁴ Kama vile mzee Daktari Bosworth alivyozea kusema, “Unaweza kuchukua yai la kuku na kuliweka chini ya kitoto cha mbwa, yataangua kifaranga cha kuku.” Kwa nini? Kwa sababu hilo ni yai na lina mazingira yanayofaa.

⁸⁵ Sijali kama wewe ni Mmethodisti, Mbaptisti, Mpresbiteri; katika mazingira mazuri, yataangua mtoto wa Mungu aliyezaliwa upya. Mazingira ndiyo yanayofanya jambo hilo, haidhuru una kibandiko cha dhehebu gani.

⁸⁶ Nilikuwa nikichunga ng’ombe. Nilimwona mlinzi wa misitu wakati tungewapeleka msituni, kutoka—kutoka malishoni huko kwenye ranchi, na kuwaingiza msituni. Yeye angesimama pale na kuangalia walipokuwa wakipita kwenye lango, kwenye ua wa mbao. Yeye hakushughulika sana na chapa, kwa maana kulikuwa na chapa za kila namna zilizopitia pale. Lakini kuna kitu kimoja alichoaangalia, kile kibandiko cha damu. Ilibidi awe ni Hereford wa asili bora la sivyo asingeingia kwenye msitu ule, kwa maana Shirika la Hereford ndilo linalowalishia kwenye msitu huo. Hana budi awe na kibandiko cha damu, kuhifadhi uzalishaji halisi.

⁸⁷ Nami nafikiri ya kwamba hivyo ndivyo itakavyokuwa kwenye Siku ya Hukumu. Yeye hataniuliza kama nilikuwa Mmethodisti, Mbaptisti, Mpentekoste, ama Mpresbiteri, bali ataangalia kile kibandiko cha Damu. “Nitakapoiona ile Damu nitapita juu yenu.” Jambo ndilo hilo.

⁸⁸ Kwa hiyo tunaona kwamba mabirika haya, baada ya kukaa kwa muda kidogo, yananinii. . . yanatuama wala hayafai. Na yanakuwa basi, pia, yanakuwa ni makazi ya vyura na mijusi na nyoka na vijidudu na bakteria, na kadhalika, kwa sababu yako kwenye hali ya kutuama. Ungeweza kuwazia, kuoshwa kwa paa la ghala, ama kutoka kwenye nyumba iliyo karibu na ghala, ama mahali popote uchafu huo ungekuwa, ni vijidudu na bakteria za namna gani, na kila kitu, kinachochukuliwa na maji na kuingiza kwenye birika hili?

⁸⁹ Sasa, ni mfano mkamilifu wa namna yoyote ya mfumo wa kujitengezeza. Mwanadamu ni kitu kilichoshindwa, tangu mwanzo. Hiyo ndiyo sababu anahitaji Mwokozi. Asingeweza kujiokoa, hawezi kujifanyia jambo lolote kwa hilo. Amepotea, tangu mwanzo. Anazaliwa ulimwenguni, mwenye dhambi, anakuja ulimwenguni akisema uongo. Yeye ni mwongo, kwa kuanzia, kwa hiyo anawezaje kamwe kujifanyia jambo lolote? Mtu mtakatifu anawezaje?

⁹⁰ Hakuna mtu mtakatifu. Hakuna kanisa takatifu. Ni Roho Mtakatifu! Si kanisa takatifu, watu watakatifu; ni Roho Mtakatifu miongoni mwa watu, hivyo ndivyo ilivyo. Amina. Si mlima mtakatifu ambapo Petro na hao wengine walisimama;

mlima huo haukuwa mtakatifu. Bali ni Mungu mtakatifu, juu ya mlima huo, aliyeufanya kuwa mtakatifu. Si mtu mtakatifu; ni Roho Mtakatifu anayetumika katika mtu huyo, ndiye anayekifanya kitu kitakatifu. Si mtu huyo, bali ni Utu wa Roho Mtakatifu! Si huyo mtu; kwa sababu, yeye ni mwanadamu tu, “aliyezaliwa katika dhambi, akaumbika katika uovu, akaja ulimwenguni akisema uongo.”

⁹¹ Mfumo wowote wa kujibunia utamweka moja kwa moja katika hilo; atapofusha kitu hicho kwa akili, macho ya kiakili, ambapo wanawazia, “Mimi ni mfuasi wa kanisa, jina langu liko kwenye kitabu. Nimefanya jambo *hili*. Baba yangu alikuwa *hivi*, na kadhalika.” Hilo linasikika sawa; ambalo, ndivyo lilivyo, sina la kusema dhidi yake. Lakini hata hivyo, rafiki, Yesu alisema, “Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi hata kuona,” *kuona*, pale, halimaanishi ya kwamba anaona kwa macho yake, bali, “*kuufahamu* Ufalme wa Mbinguni.” Mpaka utakapozaliwa humo!

⁹² Mwinjilisti huyu wa Kibaptisti angeweze, mtu huyo aliyesimama pale na kukosoa na kudhihaki Hilo angeweze? Unaona, hakuna kitu ndani yake ambacho kingeweza hata kulipokea; bali ilimbidi Mungu kufanya jambo hilo, unaona. Mungu alimpa Roho Mtakatifu. Alidhihirisha ya kwamba hili halikuwa ni unafiki, hili ni Neno. Yeye analisikia tu kutokana na wazo la shuleni, nao wanajaribu kuchukua ninii zote—baraka za Mungu na kuziweka kwenye siku iliyopita.

⁹³ Mhubiri kijana wa Kibaptisti, hapa si muda mrefu uliopita, ambaye ameketi papa hapa asubuhi ya leo; naye alinijia, na kusema, “Ndugu Branham, kuna jambo moja unalofanya ambalo ni kosa.”

Nikasema, “Nisaidie.”

⁹⁴ Naye akasema, “Wewe ni, nafikiri wewe ni mtu mwaminifu na mtu mzuri, lakini . . .”

Nikasema, “Asante, bwana.”

Akasema, “Lakini kuna kosa moja unalofanya.”

Nikasema, “Natumaini Bwana anapata kosa moja tu.”

⁹⁵ Naye akasema, “Vema, kuna ninii . . . Hili ndilo kosa unalofanya.” Kasema, “Unajaribu kuingiza ulimwenguni huduma ya kimitume, na,” akasema, “huduma ya kimitume ilikwisha pamoja na mitume.”

⁹⁶ Nikasema, “Kama Mbaptisti kwa Mbaptisti, ningetaka kukuuliza swali moja.”

Kasema, “Lipi?”

⁹⁷ Nikasema, “Je! unaamini Neno la Mungu limevuviwa, kila sehemu yake?”

Akasema, “Mbona, hakika.”

⁹⁸ Nikasema, “Basi, Yeye alisema, ‘Usiongezee neno moja, wala kuondoa Moja.’ Kwa kuwa,” nikasema basi, “Nitakuonyesha ambapo Baraka za kimitume zilipowajilia watu, kwa ahadi ya Mungu, sasa wewe nionyeshe ahadi ya Mungu na ni lini ilipowaacha watu. Unaona, kama huwezi kutoa hilo katika Neno, basi—basi sahaui jambo hilo, unaona.” Nikasema, “kwa sababu ingali inaendelea.”

⁹⁹ Hakusema kitu kwa dakika chache. Na kwa hiyo nikasema, “Vema, basi, ndugu, ningetaka kukuuliza jambo hili. Petro aliuleta ujumbe wa kimitume, kwenye Siku ya Pentekoste. Nasi sote tunajua jambo hilo ni kweli, kwa kuwa alikuwa na funguo za Ufalme, ambazo Yesu alikuwa amempa. Na sasa angalia yale aliyosema. Alisema, ‘Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo mpate ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa wale walio mbali, na kwa wote watakaotwa na Bwana Mungu wetu.’ Basi kama kuna mahali ambapo Yeye aliiondoa, basi ilikuwaje kwa maneno ya Petro kwenye Siku ya Pentekoste?” Unaona? La, haijakoma!

Ewe Mwana-Kondoo unayekufa, Damu yako
ya thamani

Kamwe haitapoteza Nguvu zake,
Mpaka Kanisa lote la Mungu lililokombolewa
Litakapookolewa, lisitende dhambi tena.

Ndipo katika wimbo mzuri na mtamu zaidi,
Nitaimba Nguvu Zako za kuokoa,
Wakati maskini ulimi huu unaopiga kitembe
na kugugumiza
Utakapolazwa kimya kaburini.

¹⁰⁰ Mungu na anisaidie kuamini jambo Hilo na kulishikilia, pamoja na sisi sote, na kulitetea, kwa sababu ni Kweli ya Injili! Naam, bwana.

¹⁰¹ Mtu mwenye hekima hapaswi kamwe kuyaangalia mambo haya. Na kujua kwamba hayatafanikiwa. Kamwe hayajafanikiwa. Dini ya kimadhehebu na ujuzi wa kimadhehebu hautafaa kabisa Mbele za Mungu. Hauna budi kuja, bila kughoshiwa, kutoka kwa Mungu. Haujawahi kutumiwa na Mungu, hakuna wakati huko nyuma ambapo Mungu aliwahi kutumia mfumo kama huo. Sasa unaninii, loo, unapata wafuasi na mambo kama hayo. Lakini ninamaanisha mbegu halisi ya Mungu, Baraka kama zile zilizoshuka kwenye Siku ya Pentekoste, kamwe haziji kwa madhehebu; zinakuja kwa kuzaliwa, kuzaliwa mara ya pili.

¹⁰² Tumealikwa kuwachukua Israeli kama—kama mfano, ambao wamekuwa. Angalia, “Wamemwacha Yeye, chemchemi yao waliyopewa, na walikuwa wamejichimbua mabirika.” Ungeweza kuwazia ja—ja—ja—jambo, wakati mtu akiwa yupo

kwenye kisima kinachobubujika, akinywa maji, na halafu anataka kujichimbia birika, unaona, apate kulinywea? Sasa hilo ndilo nabii alilosema, hivyo ndivyo Neno la Mungu lilivyosema. Hivyo ndivyo Mungu alivyomwambia nabii. “Mmeniacha Mimi na—na mmeniacha Mimi, chemchemi ya maji ya uzima; nanyi mmejichimbia mabirika, ambayo yamepasuka, nayo yanavuja.”

¹⁰³ Hebu angalia, kitu fulani, walitaka kitu fulani ambacho wangeweza kukidhibiti, ama kuonyesha yale waliyokuwa wamefanya. Huo—huo ndio ujinga wa dini ya kimadhehebu. Daima inajaribu, lazima inawabidi wawe na jambo fulani mle. Wanataka kwa vyovyote wawe na mifumo hii yote na mashirika, na kadhalika. “Na mimi ni mfuasi wa *hili* sasa.” Badala ya kuwa tu watoto wanyenyekevu wa Mungu, wanataka jambo fulani ambalo wangeweza kujionyesha. Badala ya kumwacha Mungu kulifanya apendavyo, walitaka kulifanya wapendavyo. Na hivyo ndivyo mifumo imelifanya kanisa leo. Sio . . . Kila mfumo, mmoja unataka jambo liende jinsi *hii*, mwingine unalitaka jambo liwe jinsi *ile*. Kama wewe ni Mmethodisti, huna budi kuwa *hivi*. Mbaptisti, *hivi*. Mpresbiteri, Mkatoliki, yeyote yule, wana mifumo yao. Sipingi hilo, bali hilo silo ninalozungumzia.

¹⁰⁴ Mwanadamu anataka njia yake ya kulifanya, na Mungu ana njia Yake ya kulifanya. Naye alisema, “Mnashikilia njia yenu, birika lililopasuka; wala hamtaikubali njia Yangu, njia ya Uzima.”

¹⁰⁵ Na hilo ni jambo lile lile kama lilivyo leo. Halijabadilika hata kidogo. Wazia ni ujinga jinsi gani mtu kuacha kisima cha chemchemi ya maji safi na mazuri yakibubujika, kisha anataka kwenda kwenye birika linalovuja alilojichimbia mwenyewe, na kujichimbia birika, likiwa na uchafu huo uliookotwa kutoka juu ya paa la ghala na kuingizwa mle, kisha mtu analinywea hilo. Hakika ubongo wa mtu huyo una kasoro.

¹⁰⁶ Na wakati mtu atashikilia wazo la ki—kidini la Maandiko, badala ya kumkubali Roho Mtakatifu ambaye huyathibitisha Maandiko na kuyafanya halisi kwako, kuna kasoro fulani ya kiroho kwa mtu huyo. Hiyo ni kweli kabisa. Hakika, Roho Mtakatifu! Kila mtu ana fasiri ya Biblia yao, kile unachowazia ni kweli. Mungu hahitaji msaada wako. Mungu hahitaji tafsiri yako.

¹⁰⁷ Mungu hujifasiria mwenyewe. Mungu hujifasiria jinsi Yeye—jinsi Yeye anavyosema angelilifanya. Bwana alisema hapo mwanzo, “iwe nuru,” na ikawa nuru. Hilo halihitaji fasiri yoyote. Hivyo ndivyo Mungu alivyofanya. Alisema “bikira atachukua mimba,” alichukua. Hilo halihitaji fasiri yoyote. Alisema “ataimwaga Roho Yake juu ya watu wote,” aliimwaga. Halihitaji tafsiri yoyote. Mungu hulitafsiri Neno Lake Mwenyewe kwa kulithibitisha, na kulidhihirisha, na kulihakikisha.

¹⁰⁸ Hivyo ndivyo nabii alivyothibitishwa kuwa ni wa Mungu. Yeye alisema, “Akiweko mmoja kati yenu, ambaye ni wa kiroho ama ni nabii, Mimi Bwana nitajitambulisha kwake kwa maono, nitasema naye katika ndoto. Na yale asemayo yakitimia, basi mwogopeni huyo; bali kama hayatimii, msimwogope.”

¹⁰⁹ Hilo ni jambo lile lile wakati Mungu anaposema Neno Lake, naye mtu anasema, “Neno ndilo *Hili*,” nalo linatimia namna hiyo, basi ni Mungu anayefanya jambo hilo.

¹¹⁰ Lakini kama akisema, “Ni *hivi*, na siku hizo zimepita,” mbona inachukua ninii yote... Anachukua mkate wa njaa, mkononi mwake, kwa watoto, na kuwanyang’anya; nao wanakufa kwa njaa. Mbona ungetaka kunywea birika wakati hiki kisima cha maji yanayobubujika kilikuwepo?

¹¹¹ Chemchemi ya Uzima ni nini sasa? Chemchemi ya Uzima ni nini, chemchemi ya Maji ya uzima? Kisima cha maji yanayobubujika, tungeilinganisha.

¹¹² Sasa nawatakeni mwone tofauti kati ya birika na kisima cha maji ya uzima; kisima cha maji yabubujikayo, na birika chakavu linalovuja kule nje lililojaa wadudu, mijusi, vyura, bakteria, chochote kile, unaona.

¹¹³ Na hiki hapa kisima cha maji yabubujikayo. Sasa angalia jambo hili. Kinajitegemea. Haikubidi kuchukua mifumo yoyote mikubwa na kuingiza pesa nyingi sana kwake. Haikubidi kuwaingiza wafuasi wengi sana. Kinakidhi wafuasi wake, wenye Roho wa Uzima ndani yao, akitenda kazi.

¹¹⁴ Angalia maji yanayotoka ndani yake, ya chemchemi, safi na meupe. Si birika, kitu ambacho kimetuama ambacho kimeshindiliwa mambo na watu arobaini, hamsini mbalimbali, wakisema, “*Hili* ni kweli, na *lile* ni kweli, na wazo *hili*,” na kupiga kura na kuitana, na jinsi wanavyofanya, na halafu wanaunda madhehebu kutokana na mambo hayo. Ni Neno la Mungu safi lisilo na doa na lisiloghoshiwa, likitoka mkononi mwa Mungu. Ni kisima halisi cha maji yabubujikayo.

¹¹⁵ Angalia, siri ya nguvu zake zimo ndani yake. Mwanadamu hawezi kuipata. Namna fulani ya presha, chini yake, inayokifanya kusukuma juu.

¹¹⁶ Ninakumbuka wakati mimi, nilikuwa na mazoea ya, nilipokuwa bwana nyama wa mkoa wa Indiana. Nilikuwa nikipitia kule, katika Wilaya ya Harrison, kisima fulani, chemchemi fulani. Ilikuwa daima ikibubujika. Na ninii tu, loo, ilionekana kana kwamba ilikuwa ndicho kitu chenye upeo wa furaha. Kama theluji ilikuwa ardhini, barafu, imeganda, kuwe baridi jinsi gani, ingali ilibubujika; ambapo mabwawa na matangi ya kujitengenezea ya zamani, yakiwa na vyura na kila kitu, yako huko nje yameganda, magumu.

¹¹⁷ Na hilo linaonyesha ya kwamba madhehebu yoyote, kwa ukosefu kidogo wa Roho ama badiliko dogo la angahewa, yataganda. Lakini kisima cha Mungu kinachobubujika, Yeye ni ninii—ni yeye yule jana, leo, na hata milele, kinadumisha vitu vyote vikibubujika kutoka kwake na kutupwa nje yake. Wala hakuna kitu mle ndani, kwanza. Na kitu chochote kinapoingia ndani yake, itakisukuma ikitoe njiani.

¹¹⁸ Kitu hicho kilikuwa kikibujika namna hiyo, nami nikasema, niliketi chini pale siku moja, nikawazia, “Ninaamini nitazungumza na chemchemi hiyo, kwa muda kidogo tu.” Nikavua kofia yangu, na kusema, “Kitu gani kimekufurahisha jinsi hii? Kwa nini unabubujika namna hii? Labda ni kwa sababu ayala wanakunywa kutoka kwako, mara kwa mara.”

Kama kingaliweza kunena, kingalisema, “La.”

Nikasema, “Labda ni kwa sababu ninakunywa kutoka kwako.”

“La, sivyo.”

¹¹⁹ Nikasema, “Vema, ni kitu gani kinachokufanya bila dosari hivi, mweupe? Kwa hiyo ni kitu gani kinacho—kinachokububujika, kinachokufanya ububujike, umejaa furaha wakati wote, wala hakuna kitu kinachoweza kukugandisha? Unajirusha hewani, wala hakuna kitu chochote; maji safi.”

¹²⁰ Kama kingaliweza kunena nami, je! mnajua kisima hicho kingalisema nini? Kingalisema, “Ndugu Branham, si mimi ninayebubujika, ni Kitu fulani nyuma yangu, kinachonibubujika.” Na hivyo ndivyo ilivyo. Hilo ni neno hafifu, bali mnajua ninachomaanisha.

¹²¹ Na hivyo ndivyo ilivyo kwa tukio la kuzaliwa mara ya pili. Huwezi kulizua. Ni ki—kisima cha maji kilicho ndani yako, kikibubujika Uzima wa milele. Unaona, kuna jambo fulani kuhusu jambo hilo, ambalo huna uhusiano wowote nalo. Matangi ya kujitengenezea huenda yakaganda, nayo yakiomba yapate uamsho na kila kitu; bali mtu aliye chini ya Chemchemi hiyo, anayeishi ndani ya Chemchemi hiyo, ni mchana na usiku! La, haikubidi kungojea mvua za maeneo hayo na uamsho wa mahali hapo. Umejaa Huo. “Nitampa chemchemi ya Uzima, ndani yake, inayobubujika.” Kuna jambo fulani ndani Yake, ambalo ni jipya kila siku, lisiloghoshiwa na safi. Ni Neno lisiloghoshiwa la Mungu ndani ya moyo wako na mdomo wako, likijithibitisha Lenyewe, likijinenea Lenyewe. Sijali kama kunanyesha, kama barafu inaanguka, kuna hali gani ya hewa, ungali una furaha kwa sababu Roho Mtakatifu yuko mle ndani akibubujika. Ni Nguvu zilizofichwa. Angalia. Loo, siri Yake iko ndani yake.

¹²² Inajitoa yenyewe, bure, kwa yeyote atakayekunywa na kutumia utajiri wake. Sasa huamui tu, useme, “Vema, sasa inanibidi tu kwenda kwenye kanisa la Kimethodisti kwa sababu

mimi ni Mmethodisti, kwa ajili ya ufufuo. Itanibidi kwenda *huku*, bali (kama) inanibidi kuwa Mpentekoste kwa sababu mimi ni mwanauamsho wa Kipentekoste.” Ninakwambia, wakati ukiwa na kisima hicho cha Maji yakibubujika, Chemchemi hiyo, wakati unaponywea hapo, hakuna tofauti, unayatoa kwa kila kitu kinachokaribia pale. Uko tayari kumpa Mkatoliki, Mprotestanti, Myahudi, kafiri, ama yeyote yule tumaini la Uzima. Wewe kweli, kweli una Kitu ndani yako, kinachofanya jambo hilo.

¹²³ Unaona jambo lingine kuhusu jambo hilo, haikulazimu kuyasukuma. Haikubidi kuyavuta, kuyapampu. Nimeona mengi sana ya mambo hayo mpaka yananichefua, kupampu kitu fulani; kucheza muziki chungu nzima, na kurukaruka, ama—ama lundo kubwa la maandishi huko nje mjini, na vibao vikubwa mno vya matangazo, “Mtu wa Majira Haya.”

¹²⁴ Kuna Mtu mmoja tu wa majira haya, na huyo ni Yesu Kristo, Ambaye ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Kuna Mjumbe mmoja tu kutoka kwa Mungu, na huyo—huyo ni Yesu Kristo. Naam, bwana.

¹²⁵ Haikubidi kupampu jambo Hili, wala kulivuta chini. Wala, sio, haikubidi kujiunga Nalo. Wewe lichukue tu, bure. Amina. “Mimi ndimi Chemchemi ya Maji ya uzima; mliniacha Mimi, kwenda kujitengenezea magari fulani.” Sasa haiwabidi kuyapampu, kuyapampu, kuyavuta, wala kujiunga Nayo, kuyachimba, hakuna kitu kingine. Inakubidi tu kuyanywa, bure.

¹²⁶ Huhitaji theolojia yoyote ya kujibunia kwa ajili ya kitambaa cha kuchujia, wala, kukwambia jinsi ya kupitia ndani Yake, cha kuyafanyia. Hakuna. Theolojia fulani ya kujibunia ya mfumo fulani wa kielimu, dini ya kujifanya mwenyewe mwenye haki katika *hili*, katika *hili*, ama birika fulani la mfumo wa kidini; huuhitaji. Si lazima huo uwepo. Ukiweka kitambaa juu ya Hiyo, itakitupilia mbali hewani. Haina uhusiano wowote nacho. Inajitegemea! Ni nguvu za Mungu zikichipusha Uzima. Kwa sababu gani mtu aache kitu kama Hicho, akajiunge na mfumo fulani, ni zaidi ya yale ningaliweza kusema. Haihitaji chujio lolote la kitambaa. Hailihitaji. Haihitaji kute... haihitaji kutegemea mvua za maeneo hayo ipate kujaa. Imejaa wakati wote. Amina.

¹²⁷ Mtu fulani, ninawasikia wakisema, “Mimi nimeanguka chini kwenye takataka leo.” Loo, jamani!

¹²⁸ Loo, ninafurahia kuishi katika Uwepo wa Mungu, iwe kama mambo yanaenda sawa ama hayaendi sawa. Yeye ni Uzima wangu. Amina. Yeye ni Uzima wetu. Yeye ndiye huo Uzima, Uzima tele. Naam, bwana. Na—na angalia jinsi Hiyo inavyotufanyia. Nguvu Zake na usafi Wake hudumu ndani Yake.

Haihitaji kutiwa maji yoyote kutoka kwenye birika wala mfumo mwingine wowote.

¹²⁹ Mtu fulani anasema, “Vema, una kadi gani ya ushirika? Hebu tuone kama wewe ni Mbaptisti mzuri. Nitaona kama una kadi. Ama—ama, Mpentekoste mzuri, kama wewe ni wa Umoja, Uwili, Utatu, ama—ama chochote kile tena.” Unaona, haihitaji kutiwa maji kokote. Inaendelea daima. Naam.

¹³⁰ Unajua, nilikuwa na birika hili la zamani, ilinibidi kujaza maji mle na kujaza na kuyajaza na kuyajaza, kwa pampu hii ya zamani ya kuvutia, kuyatoa mle; mwajua, kumimina maji zaidi ndani yake, na kumimina tu rundo la wadudu na kadhalika mle ndani, kutoa wadudu na kadhalika. Hivyo ni kama tu vile ilivyo kwa baadhi ya miamsho hii ya kimifumo.

¹³¹ Lakini, Mungu ashukuriwe, “Ipo Chemchemi iliyojaa Damu, ambapo wenye dhambi hujitumbukiza ndani ya gharika hiyo!” Hufanyi watu kuwa wafuasi wa kanisa, unawafanya Wakristo wakati wanapokuja kwenye Chemchemi hiyo.

¹³² Kwa nini uiache Chemchemi ya maji yaliyo hai, ukanywe kwenye shimo la maji machafu kama hayo?

¹³³ Hakuna kuyasukuma kwa pampu; nguvu Zake zimo ndani Yake. Haihitaji kuongezewa maji, naam, bwana, kwa kuwa (Yenyewe) Uzima Wake Yenyewe umo ndani Yake. Hivyo ndivyo mbegu ya Mungu ilivyo ndani ya moyo wa mwanadamu. Uzima wa Mungu umo ndani ya mtu binafsi, sio katika kanisa. Ndani yako, umo ndani yako, wewe ndiwe uliye na chembe ya Uzima ndani yako.

¹³⁴ Ladha Yake moja tu inawashawishi makasisi wa kila namna. Mwulize kasisi wa Kikatoliki, mwulize Mbaptisti, chochoote kile. Ladha moja tu ya maji haya baridi mazuri ya kisima kibubujikacho, nawaambia, inashawishi kwamba ni Kweli. Nafsi yako iliyo na njaa, kwa vyovyote vile, inamshawishi mwenye kiu, kwa kila hali. Sasa kama wewe huoni kiu... Maskini Mbaptisti huyu, hakuwa akiona kiu, kwanza; bali alipoona kiu, maji hayo yalikuwa na ladha nzuri mno. Hiyo ni kweli, lakini huna budi kuona kiu, “kiu cha heri,” kama Yesu alivyokiita hicho. “Heri ninyi mnapoona njaa na kiu ya haki, kwa kuwa mtashibishwa.” Naye Yesu alisema hivyo, rafiki. Naam, bwana, ni Chemchemi iliyobarikiwa kwa mwenye kiu.

¹³⁵ Kwa nini mtu yeyote atake kukibadilisha kwa kinamasi? Ni vipi utake kubadilisha kisima kibubujikacho kwa maji ya kinamasi, kilichojaa wadudu na uchafu wa kila namna ya nadharia za kujibunia, ambazo Mungu alisema ya kwamba, “Kuongezea moja kwenye Neno Lake, au kuondoa moja ya Maneno Yake, sehemu yake ingeondolewa kwenye Kitabu cha Uzima”?

¹³⁶ Na Mungu alipoahidi ya kwamba angethibitisha Neno hili kwa kila kizazi, “Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu na kwa

watoto wenu, na kwa hao walio mbali, kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu,” kwa nini uvute kwenye pampu ya kimfumo ambayo imeambukizwa vijidududu kwa miaka kadhaa, kutoka kwenye mana fulani ya kale? Labda mana hiyo ilikuwa ni sawa, hakuna kitu dhidi yake, katika siku za Martin Luther, katika siku za *huyu* na siku za *yule*, na hao watengenezaji wengine, hakuna neno dhidi yake; bali hiyo ni mana iliyoanguka siku nyingi zilizopita.

¹³⁷ Kama tukiangalia kwenye Biblia, ya kwamba iliwabidi kuiokota kila siku. Iliwabidi kuokota mpya. Baada ya kuchakaa kidogo, ilioza. Haiwezi kuoza bila ya kupasuka. Lazima iwe na bakteria ndani yake, ama kitu fulani ku—kuifanya ioze. Tunajua hiyo ni kweli.

¹³⁸ Na ndivyo ilivyo kwa mifumo! Baada ya kukaa hapo kutoka kwenye uamsho mmoja mkubwa hadi mwingine, na yanaambukizwa na kujaa vijidudu, na kama birika lililojaa vifurukuta-mikia, kama tulivyozea kuwaita, wadudu wadogo waliojifurukutisha mle ndani.

¹³⁹ Na hiyo ndiyo shida kwa ujuzi wa watu wengi sana siku hizi. Wa—wamejaa vifurukuta-mikia, wakifurukutika kutoka moja kuingia lingine, na moja hadi lingine, wakisimulia hadithi zisizo na Ukweli ndani yake hata kidogo. Hiyo ni kweli, wakifurukutika kutoka moja wakaingia lingine. “Nilikuwa Mmethodisti; nikajiunga na Baptisti. Nilikuwa Mkatoliki; nikaenda nipate kuwa wa *hili*. Nilienda kuwa wa *lile*.” Ni vifurukuta-mikia tu.

¹⁴⁰ Loo, sahai jambo hilo lote, na uje kwenye ile Chemchemi (Amina!), Kisima kinachobubujika, Uwepo ulio hai daima wa Kristo! Ninamwamini Yeye kuwa Chemchemi isiyokwisha ya Uzima. Unavyozidi kumnywea, ndivyo yanavyozidi kuwa matamu, na ndivyo yanavyozidi kuwa baridi, ndivyo yanavyozidi kuwa bora, na ndivyo yanavyozidi kuwa matamu. Nimekuwa nikimtumikia sasa kwa muda wa miaka thelathini na mitatu, na kila siku inakuwa tamu zaidi kuliko ilivyokuwa siku moja kabla. Kamwe sijapata . . . Yeye alisema usingeona kiu kamwe kama tungalikunywa Maji haya. Angalia jinsi lilivyo jambo kuu. Loo!

¹⁴¹ Israeli ilifanya kama vile wengi wanavyofanya siku hizi, waliacha chemchemi ya maji yaliyo hai, kwenda kujichimbua mabirika.

¹⁴² Sasa tukizungumzia juu ya neema kwa muda mfupi tu, kwamba neema ya Mungu ni kitu gani. Tuna sheria na sheria ndogo, “Na kama hufikii kiwango hiki. . . Nina kipimo cha kidini cha kupimia; kama hufikii hicho sawasawa, inakubidi, huwezi kuingia,” na kadhalika. Lakini Mungu hutuokoa kwa neema, si kwa mwanzo wa kupimia. Unaona? Lakini Mungu, tuginena juu ya neema sasa, jinsi tu jambo hili

lilivyopata kutukia, kumnywea. Kutoka kwenye mwanzi huu wa kupimia...

¹⁴³ Kunung'unika, Israeli wenye kunung'unika. Angalia, Yeye alisema, "Nami nitawazuru tena." Angalia katika Maandiko. Angalia, Yeye ataenda kuwajaribu, kuwazuru tena. Israeli wenye kunung'unika, kwenye Bahari ya Shamu, walialikwa wamfuate kupitia kwenye maji yaliyotuma ya Kimisri, wapate kuwa watu huru. Walikuwa ni watumwa. Walialikwa kuja wapate kuwa watu huru, pamoja Naye. Wakapitia kwenye Bahari ya Chumvi, Bahari ya Chumvi; Bahari ya Shamu, hasa, wakatoke kwenye hiyo, waingie katika jangwa, wapate kuleta utengano kati yao na waigaji waliokuwa wakijaribu kuigiza hilo, bila tohara.

¹⁴⁴ Loo, hilo ndilo lililosababisha shida. Kila mmoja wao aliangamia moja kwa moja katika jang...ama moja—moja kwa moja baharini, Farao na jeshi lake. Waliwaona wanadamu wakitembea kwa Nguvu za kimbinguni, kwa hiyo walirudi huko na kujaribu kuiga jambo hilo, bila ya kuwa wamehesabiwa kwenye baraka ile. Na walipofanya jambo hilo, waliangamia. Ni kujilinganisha kwa kimwili.

¹⁴⁵ Mtu anayejaribu kufanya jambo hilo, kujaribu kuiga jambo fulani, basi anafanya kujilinganisha kwa kimwili na Mkristo halisi.

¹⁴⁶ Ndugu yangu wa Kihindi pale anajua jambo hilo. Njoni kule Bombay nanyi mtawaona watu kule, Mabaniani na kadhalika, wakilala kwenye misumari na juu ya...wakitembea juu ya gilasi na—na kutembea ndani ya moto, kuonyesha yale wanayoweza kufanya, na mambo kama...Huo ni uigizaji wa kimwili wa mtu fulani huko ndanindani msituni, anayefanya jambo hilo kumtolea sadaka mungu wake.

¹⁴⁷ Tunaona jambo hilo miongoni mwa maisha yote ya dini, miigo ya kimwili, mtu fulani akijaribu kuwa kama huyo mwingine. Kuna mfano mmoja tu unaopaswa kufanana nao, huo ni kuwa kama Yesu Kristo, aliyekuwa Neno. Na ndipo hapo Neno la Mungu linapokuja kwako, litakuwa vivyo hivyo.

¹⁴⁸ Bali Mungu aliwaongoza moja kwa moja kwenda kwenye nchi ya ahadi, hata hivyo. Walipata, pia, kila tangi, walipoanza kwenda kupitia jangwani katika safari yao sasa, baada ya wao kutengana, walikuta kwamba kila tangi lilikuwa limewakaukia, wao.

¹⁴⁹ Nawe utaona jambo lile lile, ndugu, utakapoanza safari hii ya kwenda kwenye Nchi ya ahadi. Utakuta milango imefungwa. Kama vile maskini yule mhubiri alivyosema, Mwanglikana, ama chochote alichokuwa, na, muda si muda unajua, kanisa lake lilimfukuza. Uaona, mradi tu aliwafanya wengi kumpokea Roho Mtakatifu, huo ulikuwa ndio mwisho wake.

¹⁵⁰ Na sisi...nao Israeli walikuta jambo lile lile, kama mifano, katika safari yao ya kwenda kwenye nchi ya ahadi. Matangi

yote yalikuwa yamekauka. Naam, safari yao katika kutii Neno Lake lililoahidiwa, safari yao, katika matangi, waliyakuta yamekauka. Sasa walikuta tangi—matangi yasingeweza kutegemewa, kwa ajili ya safari.

¹⁵¹ Na kama unaenda kusafiri kwa kutii Neno la Mungu, na kujaribu kujiunga na *hili* na kujiunga na *lile*, utaenda kuona kwamba hakuna tangi ulimwenguni litakalounga mkono jambo Hilo. Hata kidogo. Wewe ni mtu binafsi. Mungu hukuongoza vile tu anavyotaka kukuongoza. Ndipo, tumeona jambo lile lile leo, na matangi yote yamekauka.

¹⁵² Lakini ahadi, daima ni kweli, kwa Mungu Ambaye atatimiza ahadi Yake kwa watu Wake. Yeye aliahidi kukidhi yote waliyohitaji, kwa hiyo akafanya hivyo. Katikati ya matangi matupu, makavu, wazia tu jambo hilo; na Israeli waliokuwa wakinung'unika, jangwani, katika safari yao! Yeye alimwita kiongozi mtumishi Wake, nabii Musa, kando, naye akafungua chemchemi ya maji ya uzima, kwa Mwamba uliopigwa, kusudi watoto Wake wanaoamini wasiangamie.

¹⁵³ Katika siku hii, hilo linanena juu ya neema, kwangu mimi. Hatustahili. Jinsi ambavyo tumefanya, jinsi ambavyo tumeishi, hatustahili.

¹⁵⁴ Bali Mungu, katika siku hii, kama vile papa hapa asubuhi ya leo, angalia, kwa Mmethodisti, Mbaptisti, Mpresbiteri, Mkatoliki, na wote, Yeye amefungua Chemchemi. Waebrania 13 inathibitisha jambo hili, ya kwamba ni Yeye yule jana, leo, na hata milele. Kwa hiyo ina—inalifanya hilo kuwa ni kweli, Yohana 3:16, “Kwa maana jinsi hii, Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na Uzima wa milele.”

¹⁵⁵ Nayo iliinuliwa kwa sababu maradufu, kwa sababu watu walikuwa wakinung'unika na kutenda dhambi, nao waliumwa na nyoka na walikuwa wanakufa; na kwa ajili ya msamaha wa dhambi zao, na kwa ajili ya uponyaji wa magonjwa yao.

¹⁵⁶ Na hiyo ndiyo Chemchemi ile ile iliyofunguliwa kwetu leo, kwa ajili ya wokovu wetu na kwa ajili ya uponyaji wetu, uponyanji wa mwili. “Kwa kuwa ni yeye yule jana, leo, na hata milele.”

¹⁵⁷ Na wakati ule Mwamba ambao ulipigwa kwa ahadi ya Neno la Mungu, aliyokuwa ameamuru, ulikuwa ukitoa mabubujiko ya maji safi sana; si—si yaliyotuama, si yaliyo na vijiidudu, bali Uwepo wa Mungu Mwenyewe. Maji safi, nayo yaliwaokoa wote walioyanywa. Sasa tunajua ya kwamba hiyo ni kweli, kwa maana tunasoma hayo katika Agano la Kale, kama mfano.

¹⁵⁸ Sasa, haikukulazimu kuyavuta, kuyasukuma kwa pampu, kujiunga nayo, kuingia katika seminari kujifunza jinsi ya kuyatumia. Watakwambia jinsi ya kuyatumia kule, unaona,

“Loo, vema, wewe, kama umempokea Roho Mtakatifu, tunaamini jambo hilo, bali kwa hiyo wewe u—unalifanya *hivi*.”

¹⁵⁹ Lakini, unaona, hakuna kulidhibiti. Humtumii Roho Mtakatifu; Roho Mtakatifu anakutumia wewe, unaona. Unaona, haikupasi, haikupasi kumtumia Roho Mtakatifu; Roho Mtakatifu amekushika. Karama si kitu ambacho unakichukua, kama kisu, na kuchonga penseli nacho. Ni kujisalimisha mwenyewe kwa Mungu, na kujiondoa njiani kusudi Roho Mtakatifu aweze kukutumia.

¹⁶⁰ Angalia, haikuwabidi kamwe kuyasukuma kwa pampu wala kuyavuta, wala haikuwalazimu kuuliza, “Sasa tunayatumiaje maji haya?” Kwa sababu, walijua jinsi ya kuyatumia. Walikuwa na kiu. Walijua wafanye nini nayo.

¹⁶¹ Na ndivyo ilivyo kwa mwanamume ama mwanamke, nini, haidhuru yeye ni wa kanuni gani ya imani ama madhehebu gani. Kama anamwonea Mungu kiu, haimbidi yeye kurudi mbio kwenye seminari, kama huyu Ndugu Mwanglikana alivyofanya, ama ndugu Mwingereza, jana usiku, ilimbidi kurudi na kuulizia vipi, kwa kanisa la Kianglikana, jinsi anavyopaswa kutumia karama hii kubwa aliyo nayo, kunena kwa lugha, na jinsi inavyompasa kufanya jambo *hili*. Kwanza kabisa, wangemfukuza. Unaona? Yeye alikuwa na kiu, kwa hiyo Mungu akamjaza tu. Hivyo tu. Ni kuona kiu, halafu Yeye anajaza tu.

¹⁶² Haikubidi kujizuia kabisa, mtu akwambie jinsi ya kuitumia. Mungu humwongoza kila mtu binafsi katika ninii—jinsi anavyokutaka ufanye. Wewe ni m—mtu binafsi, wewe mwenyewe. Wewe ni sehemu ya Mungu. Hakuna mtu anayeweza kupachukua mahali pako. Wala hakuna njia ya kulazimika kumwendea mtu fulani, na kusema sasa, itanibidi “kuitumia namna *hii*,” ama inanibidi “kuitumia namna *ile*.” La, bwana. Mungu huitumia jinsi ambavyo—ambavyo anataka. Unapoona kiu, unajua vya kutosha kunywa maji.

¹⁶³ Na kama unaona kiu asubuhi ya leo, inywee, hivyo tu ndivyo unavyopaswa kufanya. Mungu alikuwa na njia aliyoiandaa kwa ajili ya kiu chao, watoto wenye kiu kumnywea Yeye bure. Naye Mungu ameandaa njia kwa ajili ya kila mwanamume na mwanamke asubuhi ya leo, ambaye anaona njaa na kiu. Labda kuna watu walioketi hapa, hawajapata kuokoka. Kuna watu walioketi hapa walio karibu kabisa na kuokoka.

¹⁶⁴ Wapo watu hapa, wanaoketi hapa kama wafuasi wa kanisa, mnataka kufanya mema, bali mnanywea hilo tangi. Kamwe hawatawaambia Kweli hizi.

¹⁶⁵ Jambo pekee, kuja, ni kuchukua ahadi ya Mungu na uje kwenye Chemchemi hiyo, ndipo Yeye atakata kiu. “Yeye anywaye kutoka kwenye Chemchemi hii hataona kiu tena kamwe.”

¹⁶⁶ Angalia sasa jinsi—jinsi alivyowaweka huru watu Wa—Wake waliopokea maji haya, kwa neema, wala si kwa mfumo wala birika la elimu. Yeye huthibitisha Neno Lake, ndiye chemchemi iletayo Uzima. Ni wangapi hapa wanaojua ya kwamba ulipokea Uzima ulipolichukua hilo Neno na Maji Yake, unajua tu kuwa ulipokea Uzima? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

¹⁶⁷ Hebu na tuchukue, vema, kwa mfano, mfano mwingine tu, ama miwili, na ndipo nitafunga tu mara moja. Si—sina budi kuwa na swichi hiyo mahali fulani. Lakini hebu angalieni. Ninaendelea tu kuzungumza, bali simaanishi kufanya hivyo. Angalia, hebu na tuchukue kwa mfano, watu kadhaa tu.

¹⁶⁸ Hebu na tumchukue yule mwanamke aliyekuwa kwenye birika la Yakobo, kisima kilichochimbwa. Huyo hapo ameketi pale. Hilo tu ndilo huyo mwanamke alilokuwa, lilikuwa ni birika hili ambapo alikuja kuteka maji. Na hapo karibu na kisima hicho alikuta, katika mandhari ndogo pale, Mwanamume ameketi pale, Myahudi. Na mwanamke huyo alikuwa ni Msamaria, ni mji wa Sikari. Na tunaona ya kwamba Mtu huyu, Myahudi huyu, alimzungumzia mwanamke huyu Neno lisilo la kawaida, kasema, “Nipe maji ninywe.”

¹⁶⁹ Basi mwanamke huyu akasema, “Tuna ubaguzi. Si—si halali Kwako kuniuliza swali kama hilo; Wewe ukiwa Myahudi, na mimi ni Msamaria.”

¹⁷⁰ Akasema, “Lakini kama ungelijua ni Nani uliyekuwa ukisema naye, ungeniomba Mimi maji unywe, Nami ningekupa maji ambayo haitakubidi kuja kwenye birika hili kuyanywa; kitakuwa ni kisima cha maji yanayobubujika ndani yako.” Angalia wakati alipopata kwamba hili limethibitika kuwa ni Kweli!

¹⁷¹ Sasa, kwanza, mtu yeyote angaliweza kusema jambo hilo. Lakini yeye alisema, “Unasema mnaabudia huko Yerusalemu, nasi tunaabudia kwenye mlima huu.”

¹⁷² Akasema, “Wokovu ni wa Wayahudi. Tunajua tunachoamini. Lakini,” kasema, “hebu nikwambie jambo moja,” kwa maneno kama haya, “si kwenye mlima huu, wala Yerusalemu. Wakati unakuja ambapo mtu atamwabudu Mungu katika Roho na katika Kweli, kwa kuwa Baba anawatafuta watu kama hao.” Akasema, “Nenda kamwite mumeo uje naye hapa.” Angalia, hapa lilithibitika. Hapa inaonyesha alikuwa kwenye chemchemi gani. Kasema, “Nenda kamwite mume wako uje naye hapa.”

Akasema, “Sina mume yeyote.”

¹⁷³ Akasema, “Umesema kweli.” Unaona, ilionekana kana kwamba ilikuwa ni hitilafu dhahiri na yale aliyokuwa amemwuliza, na aliyosema, “Nenda kamwite mumeo.”

Kasema, “Sina mume.”

¹⁷⁴ Kasema, “Umesema kweli.” Kasema, “Kwa maana umekuwa na watano, naye unayeishi naye sasa siye wako.”

¹⁷⁵ Mwangelie mwanamke huyo, jinsi alivyokuwa tofauti na makuhani wa siku hiyo! Makuhani wa siku hiyo waliona jambo lilo hilo likitukia, nao wakasema, “Huyo ni pepo, telepathia fulani, ama—ama Beelzebuli.” Unaona, walishindwa kuona Neno linaloahidi jambo hilo.

¹⁷⁶ Lakini maskini mwanamke huyo aliyajua Maandiko barabara kuliko yeyote wa hao makuhani. Akasema, “Bwana, naona ya kwamba Wewe ni nabii. Hatujakuwa na mmoja kwa muda wa miaka mia nne, tangu Malaki. Lakini,” kasema, “tumemtazamia mmoja, nasi tunajua ya kwamba kuna Mmoja anayekuja, huyo Masihi. Na atakapokuja, haya ndiyo atakayofanya.”

Yesu akasema, “Mimi Ndiye.” Amina.

¹⁷⁷ Je! uliona, aliacha ndoo yake kwenye birika la Yakobo, akakimbia kwenda mjini; amejaa kisima kinachobubujika! Alikuwa ameliona limethibitishwa kikamilifu, na Yeye alikuwa ndiye ile Chemchemi ya Uzima. Hebu nimjulisha kwenu. Aliliacha hilo; hapo alipothibitika kwamba Yeye ni Neno la Uzima. Aliliacha; naye alikuwa amegundua ya kwamba Mwamba ule ule, uliopigwa huko jangwani, ulithibitishwa kwamba upo wakati huo.

¹⁷⁸ Hebu niseme, Mungu yeye yule aliyekuwa katika siku zilizopita, ambaye tunanena habari Zake sana, Yeye yupo hapa sasa; si kwa ufahamu fulani wa kitheolojia, bali kwa ufahamu wa kibinafsi wa kuthibitishwa Kwake ya kwamba angemwaga katika siku hizi za mwisho, Roho Mtakatifu juu ya kanisa Lake. Yeye si “Niliyekuwako.” Angali ni “MIMI NIKO,” wakati uliopo, daima.

¹⁷⁹ Ndipo hilo birika likapoteza ladha yake. Na vivyo hivyo na mtu yeyote anayeanguka ndani ya nguvu za Mungu, kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, mifumo ya kimadhehebu hupoteza ladha yake. Hutaki tena hivyo vyura vilivyotuama, na mijusi, na vijidudu, na kadhalika. Unakunywa toka kwenye Chemchemi iliyo safi na nzuri, Neno la Mungu, jipya kila saa ndani ya nafsi yako. Ni vile vile sasa, wakati Neno limethibitishwa kwamba ni Kweli, lionje uone kama si kweli.

¹⁸⁰ Ingawa birika hilo lilikuwa limekitumikia kisima chake, limetumikia wakati wake vizuri; lakini, unaona, Chemchemi ya Uzima ilikuwa pale, si kisima cha Yakobo tena, kwa ajili ya kunywea kiroho. Vile walivyowazia, kama wakinywea kisima kile, mbona, ingekuwa ni sawa; bali sasa Chemchemi ile ya Uzima Yenyewe ilikuwa imeketi pale.

¹⁸¹ Sasa hatuhitaji mashirika na madhehebu tuliyokuwa nayo. Tuko kwenye wakati wa mwisho. Na Mungu aliahidi, katika wakati huu wa mwisho, mambo ambayo Yeye angefanya. Na

tunayaona mambo hayo yakitimizwa, kwa Neno. Tunasikia watu wenye nguvu za kijeshi, wakisimama, na kutetemeka, na kusema, wao, “Jambo fulani liko karibu kutukia.” Tunahisi Roho Mtakatifu akituonya ya kwamba jambo fulani liko karibu kutukia. Tunaona kila kitu kiko katika utaratibu. Basi, acha mfumo huo na uje kwenye Chemchemi. Naam, bwana.

¹⁸² Lilitimiza kusudi lake, bali sasa alikuwa uso kwa uso mbele ya Chemchemi Yenyewe.

¹⁸³ Katika Yohana 7:37-38, Yesu alisema katika siku za kumalizia kwa sikukuu ya maskani (Yeye alisema nini?), “Mtu akiona kiu, na aje Kwangu, anywe.” Moja kwa moja katikati ya kundi la wanatheolojia! “Mtu akiona kiu, na aje Kwangu, anywe. Kwa kuwa Maandiko yamesema, mito ya Maji yaliyo Hai itatoka ndani yake.”

¹⁸⁴ Hiyo hapo Chemchemi ya uzima. Hiyo ndiyo Chemchemi ambayo watu wameiacha siku hizi. Kwa ajili ya kanuni ya imani, wameiacha Chemchemi ya Maji yaliyo hai. Hebu niwatambulishe Kwake. Yeye, kwangu mimi...Nami ninafunga.

¹⁸⁵ Yeye, kwangu mimi, ndiye ile Chemchemi iliyoyaokoa maisha ya Hajiri, na yule mtoto, walipokuwa wakifa nyikani.

¹⁸⁶ Ninaamini Yeye ndiye ule Mwamba, katika Isaya 32, Yeye ni ule Mwamba kwenye nchi yenye uchovu. Yeye ni mahali pa kujisitiri wakati wa dhoruba.

¹⁸⁷ Zakaria 13, Yeye ni Chemchemi iliyofunguliwa katika Nyumba ya Daudi, kwa ajili ya dhambi. Ninaamini ndivyo Yeye alivyo. Na ninyi je? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

¹⁸⁸ Katika Zaburi 36:9, Yeye ni chemchemi ya Uzima ya Daudi. Yeye ni Maji ya utulivu ya Daudi, na malisho ya majani mabichi. Yeye ni Maji karibu na kijito, kwa Daudi.

¹⁸⁹ Katika Mwanzo 17, Yeye ni ziwa la Ibrahimu la kunyonya, El Shaddai. Lakini wakati maisha yake yalipomtoka, hata hivyo yeye... Mungu alisema.

¹⁹⁰ “Mtu mwenye umri wa miaka mia moja, jambo hili litakuwaje? Mimi ni mzee, mke wangu ni mzee, mambo haya yanawezekanaje?”

¹⁹¹ Akasema, “Mimi ni El Shaddai.” Sasa, *El* ni “lile,” na—na *Shaddai* ni “ziwa,” na Shaddai ni wingi, ambalo linamaanisha “Mimi ni Mungu mwenye maziwa.”

¹⁹² Ni kama vile mtoto mchanga anayesumbuka na ni ngonjwa, na nguvu zake zinemwishia, anavyoegemea kifiani mwa mama na kunyonya apate kuzirejesha nguvu zake. Hakika. Si kwamba tu... Wakati anaponyonya, hasumbuki tena. Kifiani mwa mama yake, anashiba wakati akipata nguvu zake.

¹⁹³ Na mtu yeyote atakayechukua ahadi ya Mungu moyoni mwake, kwamba, “Ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, wote walio mbali, wote watakaotwa na Bwana Mungu wetu wamjie,” na kuegemea papo hapo kwenye hilo na kunyonya urudishe nguvu zako. Ewe mtoto unayesumbuka, amini hilo! Ni kwa ajili ya waaminio.

¹⁹⁴ Kwa mshairi mwaminio, ninaweza kufikiria juu ya nyimbo nyingi ambazo washairi walitutafutia. Kulikuwa na mmoja wao aliyesema wakati mmoja, Yeye. . .

Kuna Chemchemi iliyojaa Damu,
Inayotolewa kwenye vena za Imanueli,
Wenye dhambi wanapotumbukizwa kwenye
bubujiko hilo,
Wanapoteza waa lao lote la hatia.

Yule mwizi aliyekuwa akifa alifurahia kuona
Ile chemchemi katika siku yake;
Hapo naomba, ingawa mimi ni mwovu kama
yeye,
Nioshwe dhambi zangu zote.

Na tangu nilipoona kijito hicho kwa imani
Kilichotiririshwa na majeraha Yako,
Upendo wa ukombozi umekuwa ndio wimbo
wangu,

Na Utakuwa hivyo mpaka nitakapokufa.

¹⁹⁵ Kwangu mimi, Yeye ni Maji ya Neno la Utengano, yanayokutenga wewe na kila kitu kilicho kinyume na Neno Lake. Ninaamini Yeye ndiye Chemchemi hiyo. Naam, bwana. Hayo, Ndiyo Maji yaliyonitenga na mabirika ya kujichimbia, yakanitia kwenye Chemchemi ya Maji yaliyo hai. Loo, rafiki, ninaweza tu. . . Unaweza kuendelea na kuendelea tu, na vitu alivyo—alivyo kwetu! Yeye ni Alfa, Omega. Yeye ni Mwanzo, Yeye ni Mwisho. Yeye Ndiye aliyekuwako, aliyeko, na atakayekuja. Yeye ni Shina na Mzao wa Daudi. Yeye ni Nyota ya Asubuhi. Yeye ni Yote kwa yote kwangu.

¹⁹⁶ Na, ndugu, dada, kama wewe hujakuwa na ni—ninii. . . Umekuwa tu ukinywa kwenye tangi hili dogo la kujitengenezea, maishani mwako mwote, kwa nini asubuhi hii usiliache tangi hilo na uje kwenye Chemchemi hii?

¹⁹⁷ Na tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja. Huku vichwa vyenu vimeinamishwa. . . [Dada mmoja anaanza kuimba katika lugha nyingine. Mahali patupu kwenye kanda. Mtu fulani anatafsiri—Mh.] . . . kwa maoni yangu, wito wa madhabahuni. Ni wangapi sasa?

¹⁹⁸ Ni—nilikuwa na wasiwasi sana, ni—nilikuwa nikiwachelewesha sana, ikanifanya kukatakata ujumbe wangu vipande vipande. Lakini ninaamini Roho Mtakatifu anawataka mpate kile ninachomaanisha. Angalieni, hakuna kitu kilicho

muhimu zaidi katika siku hii kuliko kujiweka sawa na Mungu; mnaona, vyakula vyetu vya jioni, chochote kile, chochote. Bwana yupo hapa. Sasa, nimesikia tu jambo hilo kama mara moja maishani mwangu, tangu wakati huu.

¹⁹⁹ Sasa vipi... ninyi nyote hapa, si kwamba “ni wangapi.” Nyinyi nyote hapa mnaotaka kunywa kwenye Hicho, simameni tu kwa dakika moja, kwa ajili tu ya maombi. Mungu awabariki. Bwana awabariki.

²⁰⁰ Sasa ni wangapi humu ndani, wanao—wanaosimama sasa, wangesema, kwa mkono ulioinuliwa *hivi*, “Mungu, nishukie, nijaze tu, jalia ninywe kutoka kwenye Chemchemi hii. Nami sijafanya lililo sahihi, bali na—nataka unisamehe kwa jambo hilo. Ninataka uzioshe dhambi zangu. Na ni—ni—nijalie, tangu leo, nininii tu...”? Hebu angalieni! Jamani!

Kuna Chemchemi iliyojaa Damu,
Inayotolewa kwenye vena za Imanueli,
Na wenye dhambi wanapotumbukizwa katika
bubujiko hilo,
Wanaondokewa na mawaa yao yote ya hatia.
Wanaondokewa na mawaa yao yote ya hatia,
Wanaondokewa na mawaa yao yote ya hatia;
Na wenye dhambi wanapotumbukizwa katika
bubujiko hilo,
Wanaondokewa na mawaa yao yote ya hatia;

²⁰¹ Sasa kwa kuwa, wewe ambaye ni mwaminio Mkristo, umemkubali Kristo kama Mwokozi wako binafsi, bali wewe bado... Sasa kama hujamkubali, hiyo ndiyo Chemchemi. Ile tu ninayojua habari zake ni ile Chemchemi inayotoka kwenye vena za Imanueli. Sasa, na kama wengi wenu hapa...

²⁰² Ni kama tu vile nilivyokuwa nikizungumza hivi majuzi usiku kuhusu kifaranga huyu wa tai akitembea kwenye kitalu pamoja na vifaranga vya kuku. Wala hakujua lingine lolote ila hao kuku, lakini alijua kulikuwako na kitu fulani kumhusu yeye kilichokuwa ni tofauti na hao kuku. Ndipo mama yake akaja kumtafuta, naye akalia kutoka juu. Ulikuwa ni wito wa tai. Mnaona, ilibidi awe tai, kwanza, vinginevyo kamwe asingeutambua wito huo. Unaona, yeye...

²⁰³ Inabidi kuweko na kitu fulani mle, kilichorutubishwa, la siyyo hakitatoa Uhai. Na kama Mbegu, Neno la Mungu, limo ndani yako, Roho Mtakatifu yupo hapa sasa kuirutubisha hiyo na kuifanya halisi kwako.

²⁰⁴ Ni wangapi humu ndani hawajapokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, mngeweza kuinua mikono yenu? Pande zote, kila mahali, iweni tu waaminifu kweli, kama hujampokea Roho Mtakatifu, nawe ungetaka kumpokea, inua mkono wako. Popote ulipo, endelea kuinua mkono wako tu, kwa muda mfupi.

205 Sasa ninataka, ninyi mnaosimama huku karibu na mnawaangalia, ninataka mtu fulani aweke mikono yake juu yao.

206 Ninaamini hivi sasa moja kwa moja Roho Mtakatifu atamjaza kila mmoja wenu anayemtaka. Sasa msiwazie juu ya chakula huko nje kwenye mkahawa. Hebu na tuwazie juu ya Chakula hiki hapa. Hiki ndicho Chenyewe. Hiki ni Uzima. Mnaona, hiki ni Uzima.

207 Sasa geukeni nyuma, kila mmoja wenu, na wekeaneni mikono mmoja kwa mwingine. “Na wakaweka mikono yao juu yao!” Sasa nataka umwombee mtu huyo uliyemwekea mkono...

208 Sasa msiwazie juu ya kutoka. Msiwazie juu ya kitu kingine chochote. Wazia tu, sasa hivi, Roho Mtakatifu yupo hapa kumjaza kila mtu binafsi. Fungua moyo wako, mwaga nje maji yote ya birika, na useme, “Ewe Chemchemi ya Uzima, ingia ndani yangu. Nijaze, Ee Bwana Mungu, kwa wema na rehema Zako.”

209 Bwana Yesu, Chemchemi hiyo isiyoisha! Ninaomba, Mungu, ya kwamba utamjaza kila mmoja wao. Jalia Roho Mtakatifu ashuke hapa. Ninaomba, Mungu, ya kwamba tungsahau kuhusu mengine yote; ya kwamba Roho Mtakatifu ashuke miongoni mwetu, sasa hivi, na atatupa hayo Maji ya Uzima, bure, kutoka kila mahali. Tujalie, Ee Mungu. Wakati mwe—mwendeleo wa maombi na wimbo, vikishikana pamoja, Bwana, tukijua huo ni Uwepo Wako, Uwepo Wako wa Kiungu, tunataka kuja kwenye ile Chemchemi. Tunataka ubatizo halisi, wa kweli kwa Roho Mtakatifu. Bwana, watu hawa wanauombea. Ninaomba ya kwamba, wakati huu unaofaa sasa, ya kwamba watajazwa na wema huu wa Mungu. Tujalie, Ee Mungu. Yasikie maombi ya watoto Wako. Naomba uwajilie, naomba Nguvu za Mungu, na Roho Mtakatifu, awapitie. Tujalie, Mungu.

210 Ee jinsi tunavyokushukuru kwa ajili ya faraja, kwa Uwepo wa mwenyezi Mungu wa Mbinguni, anayesimama miongoni mwetu! Hivi sasa katika saa hii ya adhuhuri, Bwana, tulishe! Bwana, tunataka Chakula kutoka mezani Pako. Tulishe, Bwana, sasa hivi. Tulishe kwa Roho Mtakatifu, maishani mwetu. Nafsi zetu zilizokauka zinaona kiu. Kama ulivyosema katika ufasiri wa zenye njaa na ule wimbo, “Ingemwaga maji juu ya nchi yenye kiu.” Jalia litendeke, Bwana. Jalia Maneno Yako yadhihirike mioyoni mwa watoto Wako, “Maji juu ya nchi kavu, yenye kiu.” Mungu wa milele, sikia ombi la watumishi Wako, na utupe Baraka hiyo. Amina.

Loo, jinsi ninavyompenda Ye- . . .

211 Endeleeni tu kumsifu sasa. Tafuteni kujua, Roho Mtakatifu yupo hapa. Kama humpokei, ni shauri yako.

Jinsi ninavyompenda Yesu,

“Je! unanipenda kuliko hawa?”

...penda Yesu,
 Kwani alinipenda kwanza.
 Loo, jinsi ninavyompenda... (Mungu asifiwe!)
 Loo, jinsi ninavyompenda... (Vipi kama Yeye
 atakuja tu...? ...-ninii?)
 Loo jinsi ninavyompenda Yesu,
 Kwani alinipenda kwanza.
 Sitamwacha kamwe,
 Sitamwacha kamwe,
 Sitamwacha kamwe,
 Kwani alinipenda kwanza.
 Wa ajabu, wa ajabu, Yesu ni wa ajabu kwangu,
 Yeye ni Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu
 Mwenye Nguvu;
 Loo, kwa kuniokoa, kwa kunilinda na dhambi
 zote na aibu,
 Wa ajabu Mkombozi wangu, ... Lake lisifiwe.

212 Na tumwimbie huo sasa!

Wa ajabu, wa ajabu, Yesu ni wa ajabu kwangu,
 Mshauri, Mfalme wa Amani, Yeye ni Mungu
 Mwenye Nguvu;
 Loo, kwa kuniokoa, kwa kunilinda na dhambi
 zote na aibu,
 Wa ajabu Mkombozi wangu, Jina Lake
 lisifiwe!

213 Wote wanaojisikia hivyo, semeni “amina.” [Kusanyiko
 linasema, “Amina.”—Mh.] Loo, haleluya! Ninaona watu fulani
 wanafanikiwa sasa, kumpata Roho Mtakatifu.

Wakati mmoja nilikuwa nimepotea, sasa
 nimepatikana, nikiwa huru na hukumu,
 Yesu hutoa uhuru na wokovu mkamilifu;
 Kwa kuniokoa, kwa kunilinda na dhambi zote
 na aibu,
 Wa ajabu Mkombozi wangu, sifu...

Hebu na tuinue mikono yetu sasa na kweli tu-...

Loo, wa ajabu, wa ajabu, Yesu ni wa ajabu
 kwangu,
 Mshauri, Mfalme wa Amani, Yeye ni Mungu
 Mwenye Nguvu;
 Loo, kuniokoa, kunilinda na dhambi zote na
 aibu,
 Wa ajabu Mkombozi wangu, Jina Lake
 lisifiwe!

214 Je! mnampenda? [Kusanyiko linasema, “Amina!”—Mh.] Loo,
 wa ajabu! Isifiwe ile Chemchemi iliyojaa Damu, ambamo wenye

dhambi hupoteza hofu yote ya mwanadamu, hukumu yote, ni huru tu ndani Yake. Haleluya! Loo, jamani, hiyo ni ajabu kweli!

²¹⁵ Sasa tunapouimba huo tena, hebu na tuninii Methodisti wote, Baptisti, Katoliki, Presbiteri, wowote wale, tunapouimba huu, “Yesu ni wa ajabu, kwangu mimi,” hebu na tugeuke tu na kupeana mikono sisi kwa sisi, tuwe tu na mchanganyiko mzuri wa kale. Mnajua, mimi, hivyo ndivyo ninavyopenda. Haya, hebu na tuuimbe sasa tunapofanya jambo hilo.

Loo, Yesu ni wa ajabu, wa ajabu, kwangu mimi,

²¹⁶ [Ndugu Demos Shakarian anazungumza na Ndugu Branham, “Ndugu Branham, Ndio kwanza nipate habari juu ya Rais Johnson, amepolekwa haraka hospitalini akiwa na ugonjwa wa moyo, na labda tunapaswa kumwomba pamoja na taifa letu.” Ndugu wanajadiliana jambo hilo. Mtu fulani anasema, “Hebu na tungoje kwa dakika moja.”—Mh.]

Wa ajabu, Yesu ni wa ajabu, (hiyo ni kweli)

Loo, Mshauri, Mfalme wa Amani,

²¹⁷ [Ndugu Shakarian tena anazungumza na Ndugu Branham, “Samahani, samahani tena, je! unataka kuondoka hapo kwa dakika moja tu?” Ndugu Earl Prickett anaongoza kusanyiko katika kuimba, *Wa Ajabu*. Sehemu tupu kwenye kanda. Kusanyiko linaimba *Kuna Mto wa Uzima*. Sehemu nyingine tupu kwenye kanda—Mh.]

Biblia ilisema, “Waombeni viongozi.”

²¹⁸ Baba yetu wa Mbinguni, tunasimama katika haja kubwa mno kwa ajili ya kiongozi wa taifa letu, Rais wetu. Huenda kamwe asijue jambo hili, Bwana, bali Wewe unajua. Ninamwomba Ndugu Johnson, kwa kuwa anakiri kwamba yeye anakuamini Wewe. Na, Baba, ugonjwa wa moyo, tunafahamu, umemshika. Ninaomba, Mungu, yanusuru maisha yake. Tuko katika ha—hali ya wasiwasi mkubwa nchini sasa hivi, hata hivyo. Na jalia Roho Wako aje juu yake, Bwana. Na sasa hivi, hospitalini ama popote alipo, na jalia Roho Wako ashuke aje kwenye Hospitali hiyo ya Walter Reed na kuugusa mwili wake, akiyanusuru maisha yake. Bwana, mtu huyo ana presha, presha kubwa kuliko tunavyoweza kufahamu. Kwa hiyo tunaomba, Mungu, kama waaminio na kama sehemu ya taifa hili, tunamwomba kiongozi wetu, ya kwamba utamwongezea maisha, katika saa hii kuu, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.



MABIRIKA YAVUJAYO SWA65-0123

(Broken Cisterns)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulitolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumamosi asubuhi, tarehe 23 Januari, 1965, kwa ajili ya kiamshakinywa cha Ushirika wa Kimataifa wa Wafanyabiashara wa Full Gospel katika Hoteli ya Ramada huko Phoenix, Arizona, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2013 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org